# USAWIRI WA WATOTO KATIKA HADITHI ZA *MWEPESI WA KUSAHAU* NA *LIKIZO YA MKOSI*

**Na**

**Miricho Erastus Mutahi**

UNIVERSITY OF NAIROBI
AFRICANA COLLECTION

A1500338A
University of Nairobi Library Thesis
2015

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi ……………………………………….. Tarehe 12/11/15

**Miricho Erastus Mutahi**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi …………………………………………. Tarehe 12-11-15

**Dkt. Evans M. Mbuthia**

Sahihi……………………………………………. Tarehe 12/11/2015

**Bw. Josephat Gitonga**

# TABARUKU

Kwa mke wangu Catherine Mumbi na watoto wetu Ian Baaru na Olive Muthoni. Jitahidini kufikia kilele cha usomi kwa kuwa elimu ni nguvu.

# SHUKURANI

Ningependa kuwashukuru watu wote waliochangia katika kufaulisha tasnifu hii. Ingawa ni vigumu kuwataja wote, siwezi kujizuia kuwataja baadhi yao ambao bila msaada wao tasnifu hii haingekamilika.

Mwanzo kabisa nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt Evans M. Mbuthia na Bw. Josephat Gitonga kwa jinsi ambavyo walikuwa tayari kunipokea kila mara nilipowahitaji. Walinifungulia pazia na kuniangazia jinsi ya kushughulikia suala la utafiti kitaalamu. Usaidizi wao umenifaa katika kuandika kiusomi na kwa kujiamini.

Aidha, nawajibika kuwashukuru wahadhiri wote walionifundisha katika kozi hii ya uzamili na kunipa ushauri katika vikao vya mawasilisho. Hao ni Prof. Kineene wa Mutiso, Prof John Habwe, Prof Mwenda Mbatiah, Prof Rayya Timammy, Dkt P. I. Iribemwangi, Dkt Zaja Omboga, Dkt Amiri Swaleh, Dkt Jefwa Mweri, Dkt Ayub Mukhwana na Dkt Gichobi Mungania. Tasinifu hii isingekamilika bila mafunzo na ushauri wao. Asanteni nyote kwa kunivumilia na kunielekeza.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu wote tuliotiana shime kama vile akina Paul Sito, Evaline Kanyange, Zani Mwazani, Judith Kemunto, Kitangi Kilonzo, Achieng Otuoma na Benjamin Kilanga.

Nyote niliowataja na wale ambao sikuweza kuwataja, Mungu awabariki.

# IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza usawiri wa watoto katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*. Hadithi hizi za watoto zimejikita katika fasihi ya watoto. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha taswira za mtoto wa kike na zile za mtoto wa kiume, kulinganisha sifa za watoto wa kike na wenzao wa kiume na kuchunguza mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume katika *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*. Nadhariatete mbili zilizoongoza utafiti huu ni kwamba katika hadithi za watoto msichana huchorwa akiwa mwema kuliko mvulana na pili ni kuwa wasichana na wavulana katika jamii ya sasa wanajiona kuwa sawa. Nadharia ya sosholojia ya fasihi iliyotumiwa katika utafiti huu ilitoa msingi madhubuti wa kutathiminia usawiri wa watoto wa kike na wale wa kiume kwa vile imethibitika kuwa usawiri unaobainika unafungamana na hali ilivyo katika maisha ya jamii ya karne hii ya ishirini na moja ambapo inadaiwa wasichana wanaendelea kuwapiku wavulana katika nyanja mbalimbali za kijamii zikiwemo elimu na maadili. Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa katika jamii ya mwandishi mtoto wa kike anasawiriwa kwa njia chanya zaidi kuliko mtoto wa kiume. Hata hivyo, imedhihirika kuwa watoto wenyewe hawachukiani baina ya wale wa kike na wale wa kiume. Kupitia kwa utafiti huu nadhariatete zote mbili zilithibitishwa kuwa kweli. Msichana amechorwa kama aliye mwema kuliko mvulana. Imethibitishwa pia kuwa katika karne ya ishirini na moja hakuna majukumu wanayotengewa wasichana ama wavulana pekee bali wavulana na wasichana wanashirikiana kufanya kazi zozote. Mapendekezo yametolewa kuwa kuna haja ya kuchukua hatua za dharura kushughulikia maslahi ya mtoto wa kiume katika jamii. Jambo hili litamwokoa kutokana na hatari ya kubaki nyuma ya mtoto wa kike katika elimu na shughuli nyingine za kijamii. Mwishowe, tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

## YALIYOMO

Ungamo ... ii

Tabaruku ... iii

Shukurani ... iv

Ikisiri ... v

Yaliyomo ... vi

Maelezo ya istilahi na vifupisho vya maneno ... ix

**SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi ... 1

1.1 Suala la utafiti ... 4

1.2 Madhumuni ya utafiti ... 5

1.3 Maswali ya utafiti ... 5

1.4 Nadhariatete ... 5

1.5 Sababu za kuchagua mada hii ... 6

1.6 Upeo na mipaka ... 6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii ... 7

1.8 Misingi ya nadharia ... 10

1.9 Njia za utafiti ... 17

1.10 Hitimisho ... 17

**SURA YA PILI**

**HISTORIA NA NGUZO ZA KIMSINGI ZA HADITHI ZA WATOTO**

2.0 Utangulizi ............ 18

2.1 Historia fupi ya Hadithi za Watoto katika Kiswahili ............ 18

2.2 Sifa bainifu za Hadithi za Watoto ............ 24

2.3 Dhima ya Hadithi za Watoto ............ 31

2.4 Hitimisho ............ 34

**SURA YA TATU**

**USAWIRI WA WATOTO KATIKA *MWEPESI WA KUSAHAU***

3.0 Utangulizi ............ 35

3.1 Muhtasari wa *Mwepesi wa Kusahau* ............ 35

3.2 Taswira zinazobainika za mtoto wa kike ............ 37

3.3 Taswira zinazodhihirika za mtoto wa kiume ............ 40

3.4 Ulinganishi wa usawiri wa watoto wa kike na wa kiume katika *Mwepesi wa Kusahau* . 43

3.5 Mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume ............ 45

3.6 Hitimisho ............ 46

**SURA YA NNE**

**USAWIRI WA WATOTO KATIKA *LIKIZO YA MKOSI***

4.0 Utangulizi ............ 47

4.1 Muhtasari wa *Likizo ya Mkosi* ............ 47

4.2Taswira zinazobainika za mtoto wa kike ............ 50

4.3 Taswira zinazodhihirika za mtoto wa kiume ........ 54

4.4 Ulinganishi wa usawiri wa watoto wa kike na wa kiume katika *Likizo ya Mkosi* ........ 56

4.5 Mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume ........ 56

4.6 Taswira za jumla za watoto wa kike na wa kiume ........ 58

4.7 Hitimisho ........ 61

**SURA YA TANO**

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.0 Utangulizi ........ 63

5.1 Muhtasari ........ 63

5.2 Matokeo ya utafiti ........ 65

5.3 Hitimisho ........ 67

5.4 Mapendekezo ya utafiti ........ 68

MAREJELEO ........ 69

KIAMBATISHO A: Makala ya *Daily Nation*

KIAMBATISHO B: Jalada la *Mwepesi wa Kusahau*

## MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUPISHO VYA MANENO

**Fasihi ya watoto:** inarejelea fasihi maalumu inayoandikwa kwa ajili ya watoto. Fasihi hii hujitokeza kama vitabu vya hadithi za watoto. Hivyo, fasihi ya watoto ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kwa ubunifu ili kuwasilisha ujumbe ikilenga hadhira ya watoto.

**Hadithi za watoto:** inarejelea vitabu vya hadithi vilivyochapishwa vikikusudiwa kusomwa na watoto hasa walio katika shule za msingi darasa la kwanza hadi la nane.

**Watoto:** inarejelea fasiri ya kisheria nchini Kenya ambayo inatambua watoto kama watu ambao wana umri wa chini ya miaka kumi na minane. Katika utafiti huu, istilahi hii hasa inarejelea wasichana na wavulana kati ya miaka sita hadi kumi na mitatu ambao hasa wako katika shule za msingi darasa la kwanza hadi la nane na ambao ndio hasa walengwa wa hadithi za watoto zinazorejelewa katika utafiti huu.

**EAEP:** East African Educational Publishers

**JKF:** Jomo Kenyatta Foundation

**KICD:** Kenya Institute of Curriculum Development

**KLB:** Kenya Literature Bureau

**Mh:** Mhariri

**OUP:** Oxford University Press

**Wh:** Wahariri

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Fasihi ya watoto ni mojawapo wa tanzu muhimu za fasihi andishi. Tanzu nyingine ni pamoja na riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi na novela. Utanzu huu mara nyingi hutumia wahusika wanyama, mazimwi na binadamu ili kuweza kuvutia hadhira yake. Kulingana na Wamitila (2003) fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayoandikwa kwa ajili ya watoto. Fasihi ya watoto aghalabu huwasilishwa na kuhifadhiwa kama hadithi za watoto zilizochapishwa ingawa pia zipo kazi ambazo zimeandikwa katika tanzu nyinginezo kama vile ushairi na tamthilia. Ushairi ambao umeandikwa kwa ajili ya watoto wadogo huwa haujakuzwa na kuendelezwa kwa undani sana. Tamthilia zinazolenga hadhira ya watoto nazo huwa nyepesi sana kimuundo na huzingatia kanuni za kimsingi tu katika utunzi wa tamthilia. Baadhi ya tamthilia hizo zinatokana na hadithi simulizi ni kama vile *Kifimbo cha cheza* (Ahamed, 2003) na *Kesi ya Kuchekesha* (Wamitila, 2006). Fasihi ya watoto pia yaweza kuwa vitabu vya picha vya watoto. Kazi nyingi za fasihi ya watoto huwa na lengo la uadilishaji, yaani kukuza, kujulisha na kuendeleza maadili au mafunzo fulani. Lengo hili hutawala maudhui na fani ya kazi hizo.

Fasihi ya watoto huathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo au mawazo ya jamii kuwahusu watoto au itikadi ya jamii kuwahusu watoto. Itikadi hii inaathiri kwa kiasi kikubwa jinsi tunavyoteua kazi zenyewe za fasihi pamoja na matarajio tuliyo nayo kuhusu kazi hizo kwa mfano kuhusu kuandikwa kwake, maudhui yake, wahusika wake na mwelekeo wake. Kwa maoni yetu, fasihi ya watoto huathiriwa na mtazamo

wa jamii hutokana na ukweli kuwa wandishi wengi wa fasihi hii ni watu wazima wala si watoto wenyewe.

Kwa upande mwingine, usomaji wa fasihi ya watoto nao unaweza kumwathiri mtoto ama moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Matundura (2007) anafafanua haya kwa kutoa mfano kuwa iwapo kwenye matini wasichana wanaonyeshwa kila mara wao ndio wanaosaidia nyumbani huku wavulana wakiwekwa pembezoni kuna uwezekano kwamba hadhira ya watoto wanaoisoma matini hiyo wataichukulia hali hiyo kuwa kiwakilishi cha uhalisia katika jamii.
Mtafiti huyu anaendelea kueleza kuwa fasihi ya watoto husomwa katika kipindi ambacho watoto wanakua na kuamini mambo mengi wanayosoma kuwa ndiyo uhalisia wa maisha. Hii ni kwa kuwa hawana uwezo wa kuchuja ni yapi ya kuiga na ni yapi ya kutupilia mbali. Kwa mujibu wa maelezo haya, ni muhimu wandishi kutilia maanani taswira za watoto zinazojitokeza katika hadithi wanazotunga kwa ajili ya kusomwa na watoto ili kuweza kuwasilisha taswira zifaazo kwa hadhira lengwa.

Kulingana na Wamitila (2008) utanzu wa fasihi ya watoto ni utanzu ambao umepuuzwa kwa miaka mingi katika maandishi ya kihakiki. Kazi nyingi za kihakiki hushughulikia fasihi ya watu wazima labda kutokana na imani ya kuwa fasihi ya watoto haistahiki kuchunguzwa kinadharia au inahusu tu ngano za fasihi simulizi. Utafiti huu ulikusudiwa kuchangia katika kuziba pengo hili.

Katika utafiti huu, tulichunguza fasihi ya watoto inayowasilishwa kama hadithi za watoto. Hadithi hizi za watoto zinabainika kutokana na kuwa mhusika mkuu ni mtoto, lugha ni rahisi na msamiati umeteuliwa kwa makini huku mwandishi akihakikisha

kuwa dhamira kuu inawahusu watoto. Ingawa hadithi hizi hutumiwa kueleza mawazo ya mwandishi kuhusu jamii, mwandishi huitazama kazi ile kwa jicho la mtoto na kuhakikisha inaambatana na matarajio na matamanio ya hadhira ya watoto. Watoto aghalabu hutafakari mambo kwa mtazamo tofauti na watu wazima.

Utafiti huu unahusu usawiri wa watoto wa kike na wa kiume katika hadithi za watoto. Ili kupata usawiri wa watoto wa jamii ya kipindi hiki, tuliteua vitabu vya miaka ya karne hii ya ishirini na moja kwa utafiti huu. Vitabu hivyo ni *Mwepesi wa Kusahau* kilichochapishwa na Phoenix (2005) na *Likizo ya Mkosi* kilichochapishwa na KLB (2014). Vyote viwili vimeandikwa na Bitugi Matundura ambaye ni mwandishi mwenye tajiriba kubwa katika uandishi wa fasihi ya watoto. Baadhi ya kazi zake nyingine za fasihi ya watoto ni *Hazina ya Zuena na Makombo* (KLB), *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Phoenix), *Maria Analia* (KLB), *Masagia na Zimwi Mbilikimo* (Phoenix), *Masaibu ya Mfalme Tapwara* (JKF), *Sitaki Iwe Siri* (Longhorn), *Adha ya Kisauni* (Longhorn), pamoja na tafsiri ya vitabu vya Barbara Kimenye (OUP) ambavyo ni: *Musa, Musa na Mildred, Musa Mashakani, Musa na Watekanyara, Musa na Pepo, Musa Safarini, Musa na Rafiki wa Kalamu, Musa na Mpiga Kambi, Musa na Bahati Nasibu, Musa na Shamba la Shule, Musa Kwenye Sokomoko.* Baadhi ya vitabu vyake vya hadithi za watoto vimewahi kuteuliwa kwa mashindano ya kifasihi nchini zaidi ya mara moja.

Njogu na Chimerah (1999) wanatoa kauli kuwa mwandishi hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwa sababu ana maslahi katika jamii hiyo. Kutokana na kauli hii tunahisi kuwa Matundura ambaye ni msomi katika chuo kikuu, bila shaka anaelewa na pengine kuathiriwa na habari pamoja na sera zilizo nchini mwake

zinazoegemea kwenye uinuaji wa mtoto wa kike. Athari kama hizo zinaweza kushawishi uandishi wake wa hadithi katika vitabu kama vile *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*. Ukweli wa kauli hii utabainika katika utafiti huu utakaotumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kujaribu kuonyesha kuwa yanayoandikwa katika kazi za fasihi ni kielelezo cha maisha ya jamii halisi japokuwa yamefinyangwa na kuwa ya ulimwengu wa kibunifu wa mwandishi.

## 1.1 SUALA LA UTAFITI

Uhalisia katika jamii unaonyesha kwamba watoto huathiriwa katika kukua kwao na sifa za wahusika wanaowaenzi katika hadithi wanazosoma kwa vile wao aghalabu huamini mambo mengi wanayosoma kuwa ni ya kweli. Baadhi ya hadithi za watoto hutumia wahusika wanyama na mazimwi hasa ikiwa zimechota visa vya fasihi simulizi. Hata hivyo, licha ya kwamba mazimwi na wanyama hufanikisha maudhui kwa hadhira ya watoto wanaozisoma kazi hizo, kazi zinazotumia wahusika binadamu zinaweza kuwa na taathira kubwa mno kwa mtoto msomaji kwa kuwa matendo ya wahusika hao yanakaribia uhalisia wa binadamu. Ingawa tahakiki nyingi za fasihi ya watoto zimekwisha kufanywa, utafiti wa kina kuhusu tofauti za taswira ya wahusika wa kike na wa kiume katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya watoto bado haujafanywa.

Utafiti huu unalenga kuziba pengo hili kwa kuchunguza usawiri wa watoto katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

i. Kubainisha taswira za mtoto wa kike zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi.*

ii. Kubainisha taswira za mtoto wa kiume zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi.*

iii. Kulinganisha na kulinganua sifa za wahusika watoto wa kike na kiume katika *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi.*

iv. Kutathmini mitazamo ya wahusika watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume katika *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi.*

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

i. Je, ni taswira gani za mtoto wa kike zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi?*

ii. Je, ni taswira gani za mtoto wa kiume zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi?*

iii. Je, kuna tofauti gani kati ya usawiri wa watoto wa kike na wale wa kiume katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi?*

iv. Je, watoto wa kike wana mitazamo gani kuhusu wenzao wa kiume katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi?*

## 1.4 NADHARIATETE

Nadhariatete za utafiti huu ni:

1. Katika hadithi za watoto msichana huchorwa akiwa mwema kuliko mvulana.

2. Wasichana na wavulana katika jamii ya sasa wanajiona kuwa sawa.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Utafiti huu unalenga kutoa changamoto kwa waandishi wa fasihi ya watoto kutilia maanani zaidi usawiri wa mhusika mtoto ili watoto wanaosoma hadithi wajenge mielekeo ifaayo katika kukua kwao. Jinsi ambavyo wahusika watoto husawiriwa katika hadithi huathiri mielekeo ya watoto halisi wanaosoma hadithi katika kukua kwao. Aidha, watoto wakiwa na mazoea ya kusoma vitabu vinavyowasawiri watoto wenzao ifaavyo watapata ilhamu ya kusoma. Jambo hili hatimaye litasaidia kujenga mazoea ya kusoma miongoni mwa watoto.

Utafiti huu pia unatarajiwa kuwafaa wachapishaji katika mikakati ya kukuza sera zao za uchapishaji wa vitabu vya fasihi ya watoto ili kuendelea kuimarisha ubora wa vitabu vinavyochapishwa vya hadithi za watoto.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa watoto wa kike na wa kiume katika fasihi ya watoto kwa kurejelea hadithi za watoto za *Mwepesi wa Kusahau* (2005) na *Likizo ya Mkosi* (2014) zilizoandikwa na Bitugi Matundura na ndizo pekee zilizochunguzwa. Hizi ni hadithi ambazo zina wahusika wakuu ambao ni watoto.

Vitabu vyenye wahusika wanyama na wahusika wakuu ambao ni watu wazima havikuteuliwa. Kadhalika tulishughulikia tu baadhi ya vipengele vya fani hususani sifa za wahusika ambazo ndizo zilielekeza maudhui ya hadithi na usawiri wa watoto.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Sehemu hii itaangazia baadhi ya tafiti zilizofanywa kuhusu fasihi ya watoto katika Kiswahili ili kuonyesha zitakavyoufaa utafiti huu na zilivyo tofauti nao. Kulingana na Musau na Ngugi (1997) utafiti katika fasihi ya watoto ya Kiswahili hauna historia ndefu. Kulingana na Ngugi (2009), mojawapo wa tafiti za awali za fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya ni ule wa Mpesha (1996). Tafiti nyingine ni zile za Karuga (2005), Muthubi (2005), Kairu (2005), Matundura (2007) na wa Ngugi (2009). Utafiti huu uligundua kuwa isipokuwa Matundura wale wengine ni watafiti wa kike. Ugunduzi huu ulitupatia changamoto kuchangia uhakiki wa fasihi ya watoto. Mbali na tafiti hizi za tasnifu za vyuo vikuu, kumekuwa na machapisho mengine kuhusu fasihi ya watoto kama vile chapisho la Ngugi (2014) ambalo ni wasilisho lililochunguza fasihi katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia.

Utafiti wa Mpesha (1996) ulihusu fasihi ya watoto nchini Tanzania. Mpesha alichunguza ukuaji na maendeleo ya fasihi ya watoto nchini Tanzania kwa kurejelea vitabu vya hadithi za watoto vilivyoandikwa kwa Kiswahili kutoka nchini Tanzania. Katika utafiti wake, Mpesha alitambua dhima ya fasihi ya watoto katika jamii. Utafiti wa Mpesha uliufaa huu wetu kwa vile ulithibitisha kuwa vitabu vya hadithi za watoto huakisi hali halisi ya jamii na vile vile kuwa hadithi zile si ngano tu bali ni usawiri wa jamii. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa wake ulihusu ukuaji na maendeleo ya fasihi ya watoto ilhali wetu unahusu usawiri wa watoto katika fasihi ya watoto.

Karuga (2005) alihakiki vitabu teule vya hadithi vinavyosomwa katika shule za msingi nchini Kenya kwa kuchunguza fani na maudhui. Alieleza umuhimu wa fani

katika kumwezesha mwandishi huwasilisha mawazo yake kwa hadhira. Utafiti wake ni muhimu kwetu kwa kuwa ulieleza wahusika kuwa mojawapo wa sifa kuu za vitabu vya hadithi za watoto. Utafiti wake ulitupatia msukumo wa kuchunguza usawiri wa wahusika watoto. Utafiti wa Karuga ni tofauti na wetu kwa vile yeye alichunguza fani na maudhui ilhali sisi tunajikita katika usawiri wa wahusika watoto.

Utafiti wa Muthubi (2005) ulichunguza mikakati na mbinu za tafsiri katika fasihi ya watoto. Alichunguza vitabu ambavyo vimetafsiriwa au kurahisishwa ili vitumiwe na watoto kama vile *Mkasa wa shujaa Liyongo*. Ingawa utafiti wake ni tofauti na wetu, ulitufaa katika kuamua ni sifa gani za kuzingatia katika uteuzi wa vitabu vya utafiti wetu.

Utafiti wa Kairu (2005) ulichunguza uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto. Kairu alikuwa na madhumuni ya kuchunguza uzingatiaji wa sifa zinazofaa katika utunzi wa fasihi ya watoto katika hadithi fupi za Ken Walibora, kuchunguza jinsi uhalisia unavyobainika katika vitabu vya mwandishi huyu kupitia kwa vipengele vya wahusika, mandhari na maudhui pamoja na kubainisha mtindo alioutumia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake na uwiano wake katika fasihi ya watoto. Mtafiti huyu alionyesha kuwa kazi za kubuni za Ken Walibora zinaakisi uhalisia wa maisha ya watoto. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa vile yeye alichunguza mtindo na uhalisia ilhali sisi tunachunguza usawiri wa wahusika watoto. Hata hivyo ulitusaidia katika kudondoa sifa za hadithi za watoto pamoja na usawiri wa wahusika.

Ngugi (2009) alitafiti kuhusu hali ya fasihi ya watoto katika Kiswahili nchini Kenya kwa kuchunguza tabia za usomaji za watoto shuleni na hata nyumbani. Baadhi ya masuala muhimu ambayo utafiti wake uliangazia ni mitazamo ya watoto kuhusu kusoma, idadi ya vitabu vya kusoma walivyokuwa navyo, mazoea ya usomaji kwa ajili ya kujiburudisha na wajibu wa washikadau kama walimu wa Kiswahili na wazazi katika kukuza mazoea ya usomaji miongoni mwa wototo. Utafiti wa Ngugi uliufaa huu wetu katika kupata maarifa kuhusu masuala ya kutafitia kuhusu fasihi ya watoto. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa yeye alichunguza kuhusu tabia za usomaji miongoni mwa watoto ilhali wetu unahusu usawiri wa watoto katika hadithi za watoto.

Matundura (2007) alitafiti kuhusu taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Alikuwa na madhumuni ya kuchunguza ni kwa kiwango na kwa namna gani wandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wanaendeleza taswira dumifu za uana zinazoendeleza ubaguzi wa kijinsia. Alitaka kujua iwapo uendelezaji huu ni jambo linalofanywa kimakusudi au ni sadfa. Aidha alinuia kutathmini iwapo wahusika wa kike na wa kiume katika fasihi ya watoto wamesawiriwa kwa usawa au iwapo wamebaguliwa kwa misingi ya jinsia zao. Lengo kuu la utafiti wake lilikuwa kuonyesha kwamba kutosawiriwa kwa wahusika kwa njia ya usawa katika fasihi ya watoto kunaweza kuchangia katika kuendeleza taswira dumifu za uana katika jamii husika. Utafiti wake uligundua kuwa wandishi wa fasihi ya watoto wanaendeleza taswira dumifu za uana. Mtafiti huyu aligundua kuwa katika vitabu alivyochunguza mhusika wa kike amesawiriwa kama dhaifu, mtegemezi wa mwenzake wa kiume na aliyebaguliwa, mhusika wa kiume amesawiriwa kama jasiri na aliye na nguvu na uwezo.

Utafiti wetu ni tofauti na wa Matundura kwa vile utafiti wetu umejikita katika usawiri wa wahusika watoto pekee ilhali ule wa Matundura ulichunguza taswira dumifu za uana kwa kujumuisha pia wahusika walio watu wazima. Fauka ya hayo, mtafiti huyu alitaka kuchunguza jinsi taswira dumifu za uana zinavyoendelezwa na wandishi ilihali utafiti wetu ulinuia kuchunguza iwapo kuna mabadiliko ya taswira za uana kutokana na mapito ya wakati.

Hata hivyo utafiti wa Matundura uliufaa huu katika kuelekeza kuhusu namna ya kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto kwa njia mwafaka ili kutambua usawiri wa watoto.

Sehemu hii imeonyesha kuwa tafiti zinazohakiki fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya zinaendelea kushika kasi. Hata hivyo kuna pengo hasa katika usawiri wa watoto katika hadithi za watoto. Kairu (2005) anapendekeza kuwa licha ya kwamba juhudi nyingi zimefanywa kuendeleza fasihi ya watoto, kuna haja ya kuiimarisha zaidi kwa kuendelea kuifanyia uhakiki na kuitathmini ili kuibuka na miongozo na vigezo vya kutumiwa katika kuandika vitabu bora zaidi vya fasihi ya watoto. Utafiti huu unanuia kuziba pengo hili.

## 1.8 MISINGI YA NADHARIA

Sehemu hii inachunguza maelezo ya nadharia ambayo iliongoza utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya sosholojia ya fasihi.

Kwa mujibu wa Swingerwood (1975), mwasisi wa nadharia ya sosholojia ya fasihi ni Taine. Taine alisema kuwa fasihi huakisi jamii na hata alilinganisha fasihi na kioo kuonyesha kuwa fasihi huakisi maisha ya jamii kama vile kioo kinavyoakisi sura ya

mtu anayejitazama. Taine hata hivyo alikuwa ameyachukuwa, kuyaunda upya na kuyakuza mawazo ya Germaine de Stael. Kulingana na *Encyclopaedia Britannica online*, (2011) de Stael alionyesha umuhimu wa nadharia hii katika kazi yake ya *The influence of Literature upon Society* (1835). Alidai kuwa kazi ya kifasihi inapaswa ionyeshe uhalisia wa kimaadili, kihistoria, hali ya utamaduni, uchumi na siasa katika jamii ambamo kazi husika ya fasihi imeibuka.

Mtaalamu aliyechangia pakubwa nadharia ya sosholojia ya fasihi kiasi cha baadhi ya wasomi kumtaja kama mwaasisi wa nadharia hii ni Georg Lukacs katikati ya karne ya ishirini. Lukacs alikuwa ameathiriwa na mawazo ya Karl Marx kuhusu maendeleo ya kijamii na migongano ya kitabaka. Tahakiki nyingi za Ki-marx ni za kijamii na ziliendeleza maisha ya jamii kama yalivyokuwa wakati wake. Coser (1963) anasema sosholojia ya fasihi hutumiwa katika uhakiki kuthibitisha jinsi kazi ya fasihi inavyohusiana na vitengo fulani vya kijamii kama vile imani, mila desturi, maadili, elimu na muundo mzima wa jamii. Anasema kuwa fikira na ubunifu wa mwandishi huathiriwa na tajiriba yake katika jamii anayoandikia. Warren na Wellek (1973) wanasema kuwa uhusiano kati ya fasihi na jamii umejikita katika kauli aliyotoa De Bonald kwamba fasihi ni kielelezo cha jamii. Kwa hivyo ni muhimu kuichukulia fasihi kama zao la jamii na ambalo huwa limeathiriwa na mazingira ya kijamii. Mtunzi vilevile huwa ni mwanajamii na huwa anashawishiwa na hali halisi ya maisha ya wakati wake na kuizingatia katika uandishi wake. Hivyo, fasihi huwa na ufungamano mkubwa na asasi za kijamii na hivyo masuala mengi ya kifasihi huwa masuala ya kijamii. Hii inamaanisha kuwa mwandishi huchota maudhui ya kazi yake kutokana na mambo yanayotokea katika jamii yake.

Eagleton (1988) anatetea mtazamo wa sosholojia ya fasihi akirejelea istilahi yenyewe "sosholojia ya fasihi". Fasihi ni zao la jamii na hivyo inaathiriwa na shughuli za jamii. Hili ni jambo ambalo mhakiki yeyote hawezi kupuuza iwapo uhakiki wake utakuwa na mashiko. Kutokana na kauli hii tunaweza kusema kuwa mvuto mmoja unaofanya watu wapende kusoma kazi iliyoandikwa ni ikiwa watu hao wanaosoma kazi husika wajiona katika kazi ile kwa maana kuwa wataweza kuhusisha yanayotokea katika hadithi na mambo yanayotokea katika jamii yao. Wakati mwingine msomaji ataweza hata kujicheka na kisha kujirekebisha kutokana na matukio ya hadithi. Hii ni kwa kuwa fasihi inamulika jamii kutokana na maudhui yanayoshughulikiwa. Maudhui haya hujitokeza kutokana na vitendo vya wahusika, maneno wanayosema au yanayosemwa kuwahusu na hata wakati mwingine kutokana na majina waliyopewa. Maudhui aghalabu huibuka kutokana na matukio halisi yanayotokea katika jamii.

Warren na Wellek (1973) wanafafanua kuwa maudhui mengi ambayo huibuka katika uchunguzi wa kifasihi hutokana na masuala ya kijamii. Wanasema:

> Fasihi imeibuka kutokana na uhusiano wa karibu na asasi za kijamii ... fasihi pia ina dhima katika jamii na haiwezi kuwa ya mtu binafsi, hivyo basi masuala mengi ambayo huibuka kupitia uchunguzi wa kifasihi huwa ya kijamii. (Uk 94)

Wamitila (2003), anasema kuwa nadharia hii hutumiwa na wahakiki ili kuthibitisha jinsi kazi fulani ilivyoathiriwa na vitengo fulani vya mazingira kama vile tabaka la mwandishi, jinsia yake, matamanio yake, hisia, muktadha wa kiuchumi, tabaka la kijamii la hadhira lengwa na thamani za hadhira hiyo. Wamitila (2008) aneleza kuwa fasihi kama sehemu ya utamaduni wa jamii yoyote ile huhusiana, huingiliana na huathiriana na nyanja tofauti za kijamii. Anafafanua kuwa fasihi ni asasi ya kijamii kwa kuwa inatumia lugha ambayo ni zao la jamii na kwa kuwa inachota malighafi ya

maudhui kutokana na jamii. Mwandishi anayetunga kazi ya fasihi anafanya hivi katika muktadha wa jamii maalumu na kwamba anapaswa kuonyesha uelewa na utambuzi wa matukio ya jamii hiyo. Mtafiti huyu anasema kuwa fasihi ni kama mwigo au kiwakilishi cha maisha ya jamii. Sifa moja ya fasihi inayohusishwa na mtazamo huu wa nadharia ya mwigo ni kuwa fasihi na jamii zina uhusiano wa uhalisi ambao unafanana na ule wa kioo kumaanisha kuwa maudhui na wahusika katika kazi ya fasihi huakisi mambo yaliyoko kwenye jamii inayohusika. Hii ina maana kuwa wahusika wa fasihi huwa wanawakilisha watu fulani halisi katika jamii lakini kwa njia ya kiubunifu. Mambo wanayotenda, wanayosema au yanayosemwa kuwahusu wahusika hao na jinsi wanavyosawiriwa huchangia katika kukuza maudhui ambayo ni kielelezo cha maisha ya jamii husika.

Katika utafiti huu, ufafanuzi huu unamaanisha kuwa tunapoitathmini kazi tuliyoteua ya fasihi ya watoto, tunapima ni kwa kiasi gani sifa, thamani, matendo, matukio na usawiri wa wahusika watoto wa kike na wa kiume unaopatikana katika vitabu vinavyochunguzwa unafungamana na uhalisi wa jamii. Thiong'o (1978) anasema ya kwamba fasihi ina uhusiano na maisha ya kila siku ya jamii kwa kuwa haichipuki kwenye ombwe tupu. Anadai kuwa fasihi hupewa msukumo, umbo, mwelekeo na nguvu na hali halisi zinazotokana na jamii husika.

Mbuthia (2005) anaendeleza wazo la Thiong'o kuwa fasihi haichipuki kutoka ombwe tupu. Msomi huyu anaeleza kuwa mojawapo ya majukumu ya fasihi ni kuwasaidia wanadamu kuyaelewa vyema masuala wanayokumbana nayo kibinafsi na pia kama jamii. Hivyo fasihi ni chombo kinachosaidia jamii kujielewa na kadhalika kuyaelewa mazingira yake.

Kwa maoni yetu hivi ni kumaanisha kuwa mbali na fasihi kuathiriwa na jamii, fasihi kwa upande wake hali kadhalika huiathiri jamii na kuipa mwelekeo.

Ntarangwi (2004) anasema fasili nyingi za fasihi zimeegemea kuieleza katika uhusiano wake na jamii. Fasili hizi zimeonyesha kwamba fasihi ni asasi ya jamii na uhusiano wake na jamii hauwezi kupuuzwa. Akimnukuu Escarpit, R (1974:4), Ntarangwi anasema kwamba fasihi lazima ichukuliwe kama iliyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya kijamii. Fasihi ni asasi ya kijamii inayotumia lugha kuwasilisha mawazo ya mwandishi kuhusu maisha katika jamii. Kwa hivyo, fasihi huwakilisha maisha halisi ya jamii na huhusu jamii fulani. Utunzi wake hulenga jamii fulani ambayo aghalabu ni jamii ya mwandishi. Maendeleo na mabadiliko ya kijamii hutokea kuwa maendeleo na mabadiliko ya fasihi hivi kwamba hatuwezi kutenganisha fasihi na jamii inamoibukia.

Ntarangwi (2004) anazidi kufafanua kuwa wale wanaosisitiza kigezo cha fasihi na jamii, wametoa kauli kwamba pana aina mbalimbali za fasihi ambazo zinaambatana na jamii husika. Dhana kama vile fasihi ya Kirusi, fasihi ya Kiafrika. Fasihi ya Kiingereza ni baadhi ya mifano ya kazi za fasihi zinazohusishwa na jamii fulani. Fasihi kama hizi hulenga jamii fulani pana zenye kaida na maadili yanayopatana katika muundo wa kijumla. Fasihi hivyo basi, hubeba historia ya jamii. Kwa mfano, katika fasihi ya Kiswahili tunaweza kupata vipindi maalum vya historia ya jamii kama vile kipindi cha ukoloni na kipindi cha baada ya ukoloni na ukoloni- mamboleo. Hivyo fasihi na jamii ni vitu visivyotengana. Mtazamo wa fasihi kupitia sosholojia, hutufanya tumchukue mwandishi kama zao la nguvu za kisosholojia za wakati wake.

Kama nadharia nyingine yoyote, sosholojia ya fasihi ina wapinzani wake. Hawa hudai kuwa nadharia hii haitufai katika kuhakiki uhusiano kati ya fasihi na masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa vile uhusiano hauwezi kujitokeza wazi katika kitengo chochote kile na hivyo ni vigumu kutathimini umuhimu wake. Aidha, wanadai kuwa jinsi mwandishi anavyowasilisha kazi yake hutegemea uzoefu na mtazamo wake kuhusu maisha hivyo itakuwa si kweli kufikiri kuwa kazi ya mtu binafsi ni kiashiria cha maisha ya jamii kwa ujumla katika jamii anamotoka. Hata hivyo wahakiki wanaopinga mbinu ya kisosholojia hawapingi kuwepo uhusiano baina ya fasihi na hali ya kijamii kwa upande mmoja na uchumi na siasa kwa upande mwingine (Chacha, 2013).

Nadharia ya sosholojia ya fasihi ilitufaa katika kushughulikia kazi hii hasa kutokana na mihimili yake mikuu ambayo mosi ni matukio yenye kuakisi maisha halisi ya jamii na pili ni wahusika wanaotenda vitendo vinavyowakilisha matendo halisi ya watu katika jamii. Hadithi tulizochunguza, kwa mfano, zinaakisi jinsi watoto wa kike na wa kiume wanavyochukuliwa na jamii, na sifa wanazosawiriwa kuwa nazo na mwandishi. Nadharia hii basi iliufaa utafiti huu kwa kuwa matukio katika hadithi tulizochunguza yameonekana kuwa kielelezo cha hali ilivyo katika jamii ya sasa.

Msukumo wa kutumia nadharia hii katika utafiti huu umetokana na madai ya mara kwa mara miongoni mwa watu katika jamii na kupitia vyombo vya habari kuwa wasichana katika jamii ya sasa wanawapiku wavulana katika viwango vyote vya elimu. Gazeti moja la humu nchini, *Saturday Nation* Juni 20, 2015 kwa mfano, limedai kufanya utafiti ambao matokeo yake yanaonyesha kuwa baada ya miaka mingi ya kampeni za kuinua maslahi ya mtoto wa kike, wasichana sasa wako mbele ya wavulana katika nyanja za kijamii hasa elimu (tazama kiambatisho A). Inahofiwa

kuwa siku hizi wavulana wengi kuliko wasichana huacha shule kabla ya kumaliza shule ya msingi huku idadi ya wasichana wanaoendelea na masomo hadi chuo kikuu ikizidi kuongezeka sana kuliko ile ya wavulana. Washikadau mbalimbali katika elimu pia wamekuwa wakikubaliana na madai haya.

Kwa kuongozwa na nadharia ya sosholojia ya fasihi, utafiti huu basi ulikusudia kuchunguza jinsi msichana na mvulana wanavyosawiriwa katika vitabu vya hadithi za watoto vilivyoandikwa miaka ya hivi karibuni katika karne hii ili kuona kama usawiri wa kijinsia unachukua mielekeo mipya kutokana na mabadiliko yaliyoko katika jamii ya sasa ambapo msichana amewekwa mbele hata na sera za serikali katika elimu.

Tumeitumia nadharia hii kuhakiki usawiri wa watoto wa kike na wale wa kiume katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* na hadithi ya *Likizo ya Mkosi* kutathimini iwapo usawiri huu unaakisi maisha ya jamii ya karne ya ishirini na moja. Hii ni karne ambayo kwa maoni yetu jamii ya Wakenya kwa jumla, imempa kipaumbele mtoto wa kike huku mtoto wa kiume akiendelea kusahaulika. Kumekuwa pia na sheria za watoto zinazohimiza haki za watoto kama vile elimu na pia shinikizo za makundi mbalimbali yasiyo ya kiserikali yanayotetea mtoto wa kike kwa kudai kuwa anachoweza kufanya mtoto wa kiume, wa kike anaweza kufanya (na pengine hata vizuri zaidi).

Nadharia hii imetusaidia kutoa picha halisi ya jamii kwa kudhihirisha wazi usawiri wa wahusika watoto wa kike na kiume katika muktadha wa jamii zao.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Kimsingi, utafiti huu ni wa kimaelezo. Buliba (2014) anafafanua kuwa utafiti wa aina hii hueleza jinsi mambo yalivyo na hutumika sana katika tafiti zinazohusu lugha na fasihi. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Tuliteua vitabu vya hadithi za watoto tukizingatia sifa maalumu za fasihi ya watoto zilizotambuliwa. Tulivisoma kwa kina vitabu tulivyoteua vya hadithi za watoto ili kupata usawiri wa watoto wa kike na wa kiume. Baada ya kuvisoma, tulidondoa sifa za wahusika watoto ili kupata usawiri wao, tulibainisha sifa za watoto wa kiume na zile za watoto wa kike huku tukizichanganua sifa hizo kupitia mtazamo wa nadharia ya sosholojia ya fasihi na kisha tukatoa maelezo kuhusu usawiri tuliopata. Hali kadhalika tulidurusu tasnifu mbalimbali zinaohusiana na mada yetu na nadharia ya sosholojia ya fasihi ili kuona zinavyotofautiana na utafiti huu na jinsi zinavyoweza kuufaa.

## 1.10 HITIMISHO

Katika sura hii, tumefafanua mada ya utafiti wetu inayohusu usawiri wa watoto katika vitabu vya hadithi za watoto. Katika sura hii ndipo tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, nadhariatete na sababu za kuchagua mada hii zimefafanuliwa. Aidha, tumejadili upeo na mipaka, tumetalii yaliyoandikwa kuhusu somo hili la fasihi ya watoto ili kushadidia pengo la utafiti huu na kisha kufafanua misingi ya nadharia huku tukifafanua jinsi nadharia hii itakavyoufaa utafiti huu. Hatimaye, njia za utafiti zilizotumika zimefafanuliwa. Mambo haya yamekuwa kama dira ya kuongozea utafiti huu.

# SURA YA PILI

# HISTORIA NA NGUZO ZA KIMSINGI ZA HADITHI ZA WATOTO

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sehemu hii tumejadili historia na nguzo za kimsingi za hadithi za watoto. Nguzo muhimu ambazo tumejadili ni sifa bainifu za hadithi za watoto pamoja na dhima ya hadithi hizo ili kuweka wazi dhana ya hadithi za watoto.

Sifa hizi zilikuwa muhimu kwa kuwa ndizo tulizozingatia kuainisha vitabu tulivyoteua na kuvitambua kama vitabu vya hadithi za watoto. Aidha, sifa za hadithi za watoto, hasa kuhusu wahusika, zilikuwa muhimu katika kubainisha usawiri wa wahusika watoto kwenye hadithi tulizoteua. Tumejadili pia dhima ya hadithi za watoto katika jamii ya sasa. Nafasi ya hadithi za watoto katika jamii ni muhimu katika utafiti wetu hasa kwa kuwa tuligundua hadithi zina wajibu wa kuangazia masuala yanayohusu watoto katika jamii. Kadhalika, majukumu haya yalikuwa muhimu katika kutuwezesha kutathimini hadithi tulizoteua kwa mtazamo wa sosholojia ya fasihi.

## 2.1 HISTORIA FUPI YA HADITHI ZA WATOTO KATIKA KISWAHILI

Ngugi (2009) anaeleza kuwa hali ya fasihi ya watoto inatofautiana katika mataifa mbalimbali. Mtafiti huyu anaeleza kuwa katika mataifa mengi ya Kimagharibi kwa mfano, fasihi ya watoto imeimarika zaidi kuliko katika mataifa ya Kiafrika. Katika mataifa hayo asilimia kubwa ya watoto ina elimu na uwezo wa kusoma fasihi iliyoandikwa. Katika nchi za Afrika Kenya ikiwemo, ukuaji wa fasihi ya watoto

umepitia mikondo mingi katika safari yake ndefu. Kairu (2005) anasema kuwa katika kipindi cha kabla ya ukoloni fasihi hii ilikuwa simulizi. Fasihi hii ilitokana na tajriba za watu katika maisha na mahusiano yao pamoja na maingiliano katika jamii zao. Hadithi ziliwapa watoto picha halisi ya jamii zao na falsafa yao. Hadithi hizi ziliwafunza watoto maadili na kukashifu tabia mbaya kama vile ulafi, uchafu, ukatili na athari zake.

Katika kipindi cha ukoloni, fasihi ya watoto ilikuwa ikiandikwa na wakoloni wazungu. Kairu (2005) akimrejelea Mpesha (1996) anasema kuwa kipindi cha ukoloni kilileta mabadiliko ya kifasihi katika fasihi iliyosomwa na watoto. Fasihi iliyoandikwa ilihusu utamaduni wa kigeni. Fasihi hii pia ilidunisha fasihi ya Kiafrika na kuipuuza. Nia yake ilikuwa kumsawiri Mwafrika kama mtu mjinga aliyeishi kama mnyama na aliyekosa maendeleo yoyote yale. Nia yake ilikuwa kumshawishi Mwafrika kuwa utamaduni wake ulikuwa duni.

Mwishoni mwa kipindi cha ukoloni, walizuka waandishi wa Kiafrika ambao waliandika hadithi za watoto zilizosomwa shuleni. Hadithi za kipindi hiki zilijaribu kuinua hadhi ya Mwafrika kupitia mtazamo wa Kiafrika. Mifano michache ni hadithi ya *Adili na Nduguze* (Shaaban, 1952), *Lila na Fila* (Kiimbila) na *Kurwa na Doto* (Farsy, 1960).

Baada ya ukoloni fasihi ya watoto ilijaribu kujengua mafunzo ya kikoloni kuhusu Mwafrika kama mtu duni. Fasihi hii ilitilia maanani maslahi ya mtoto wa Kiafrika na tajriba zake. Baadhi ya vitabu vya watoto vilivyojulikana sana kwa kutumiwa shuleni

vilikuwa *Kaka Sungura na Wenzake* (Evans Brothers Kenya Ltd), *Nani Mjinga?* (Michuki) na *Hadithi za Furaha* (Kitula King'ei).

Jambo linalodhihirika kutokana ha historia hii ni kuwa fasihi ya watoto imeendelea kuakisi mitazamo ya kijamii na hali ya maisha katika jamii. Katika karne ya ishirini kwa mfano, hadithi nyingi zilimsawiri mtoto wa kiume kama shujaa pengine kutokana na mitazamo ya ubabedume kama anavyosema Howe (1970) katika makala kuhusu taswira dumifu za uana anapodai kuwa jamii zilifunza watoto tangu utotoni kuhusu yanayotarajiwa kutokana na jinsia yao. Kwa mfano, walishauriwa kuwa wavulana hawalii kwa kuwa ni jasiri lakini wasichana hulia kwa kuwa ni wanyonge na wenye hisia dhaifu. Watoto walifunzwa mambo kama haya na watu waliotangamana nao katika jamii wakiwemo wazazi wao, walimu, dini na hata watoto wenzao. Wanajamii walichukua mawazo haya na yakaganda akilini mwao. Mawazo ganda kama haya yalijitokeza kwa wingi katika vitabu vya hadithi zenye wahusika wakuu ambao ni watoto vya karne iliyopita. Kwa mfano, hadithi ya *Tajiri Mjanja* (Omolo, 1967), *Bonde la Wafu* (Manji, 1996), *Atendaye Mema* (Maillu, 1997) na *Androko na Simba* (Mkufya, 1998). Katika hadithi ya watoto ya *Tajiri Mjanja* iliyoandikwa mwaka wa 1967, kwenye ukurasa wa kwanza tunaelezwa:

> Hapo zamani za kale katika kijiji cha mbuga, nchi ya Waluo, palikuwa na mzee mmoja ambaye alikuwa akijulikana na watu wengi kama Mzee Buora. Mzee Buora hakuwa na bahati kwa maana alizaa watoto wengi, lakini wote walikuwa wasichana tu, katika desturi ya Waluo mtu asiyekuwa na mtoto wa kiume hudharauriwa sana na jirani zake.( Uk 1)

Madai haya ya kwamba mtu asiyekuwa na mtoto wa kiume alidharauriwa sana na wenzake yanaashiria kuwa mtoto wa kiume alithaminiwa kuliko mtoto wa kike katika jamii ya hapo awali. Mawazo sawa na haya yanatokea katika *Rosa Mistika*

(Kezilahabi, 1971) wakati mama yake Rosa anakabiliwa na tisho la kutalikiwa na mumewe iwapo hangejifungua mtoto wa kiume kutokana na mimba aliyokuwa nayo. Hapo awali alikuwa amewazaa watoto wasichana pekee.

Katika hadithi ya *Bonde la Wafu* ambayo pia iliandikwa katika karne iliyopita ajabu ni kuwa kinyume na hadithi za karne hii ambazo aghalabu huhusisha wahusika wakuu wasichana na wavulana, kitabu hiki ni mkusanyiko wa hadithi nne na zote zina wahusika wakuu wavulana pekee. Hadithi zote nne zinawasawiri wavulana hao kama wenye ujasiri mkubwa ingawa wengi wao wamesawiriwa kama wahalifu. Mathalani, hadithi ya *Bonde la Wafu* yenywe inahusu wavulana ambao wanaiba bunduki na kwenda kuwinda porini pasi na ruhusa ya wazazi wao. Hadithi ya pili ambayo ni *Musa yu Matatizoni*, inahusu mvulana kujiingiza uhalifuni kwa kutaka kuwaridhisha wenzake. Hadithi ya tatu ni *Kido* na inahusu kutekwa nyara na majambazi kwa mvulana mmoja wa shule. Nayo hadithi ya nne iitwayo *Wavamizi* inahusu wavulana waovu wanaotaka kuharibu mazingira yanayotegemewa na viumbe. Yaelekea kuwa pengine mawazo ya mwandishi, Akberali Manji, yaliathiriwa na mtazamo wa kijamii ambao ulielekea kuonyesha kama kwamba mvulana alithaminiwa kuliko msichana na hivyo alionekana kutekeleza shughuli muhimu katika jamii huku msichana akiwa haonekani hasa katika vituko vilivyohitaji ujasiri kama vile vinavyosimuliwa katika hadithi hizi. Isitoshe, kila hadithi ina michoro kadha lakini hakuna mchoro wenye picha ya msichana isipokuwa moja katika ukurasa wa 28 yenye mwanamke mkubwa. Jambo hili ni kinyume na michoro katika hadithi za watoto za siku hizi ambazo aghalabu huwa na michoro inayohusisha wasichana na wavulana na kuonyesha kuwa kile ambacho mvulana aweza kutenda hata msichana aweza pia. Katika hadithi ya *Atendaye Mema* mwandishi, David G. Maillu, anazungumzia juu ya mvulana mmoja

kwa jina Mbotela. Hadithi hii ina wahusika wakuu wavulana pekee. Wavulana wengine walikuwa Mende na Kyengo. Walikuwa wawindaji hodari. Hadithi hii pia haimshirikishi mhusika msichana kama mhusika mkuu. Hii ni ishara kwamba msichana hakuhusika katika shughuli muhimu za jamii ya kale kama vile uwindaji ambao ulikuwa ni njia ya kutafuta chakula cha kuikimu jamii. Hadithi ya *Androko na Simba* ni hadithi iliyoandikwa mwaka 1998 ambapo ni karibu na karne hii. Ingawa hadithi hii inahusisha mtoto wa kike na yule wa kiume, hatimaye yule wa kiume kwa jina Androko anaishia kuwa shujaa wakati anapofaulu kumwoa binti wa mfalme.

Katika karne ya ishirini na moja, uandishi wa hadithi za watoto katika Kiswahili umeimarika sana kifani na kimaudhui. Kukua huku kunathibitika kutokana na idadi kubwa ya vitabu vya hadithi za watoto vinavyoshapishwa na washapishaji mbalimbali. Kutokana na utafiti wetu, nchini Kenya kwa mfano, idadi ya waandishi wanaoandika vitabu vya hadithi za watoto vya Kiswahili na ambavyo vinalenga watoto wa shule za msingi imeongezeka katika kipindi cha kuanzia mwaka wa 2000. Waandishi hawa wamechagia ubora wa vitabu vya hadithi za watoto kwa kuwa wengi wao ni waandishi maarufu wa fasihi ya Kiwahili kwa jumla na wana tajriba kubwa ya Kiswahili. Wengi wa waandishi watajika ni wahadhiri katika vyuo vikuu, wengine ni walimu katika shule mbalimbali na wengine ni wasomi wenye vipawa vya kuandika.

Usomaji wa hadithi za watoto shuleni ulipata mwamko mpya baada ya Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za msingi mwaka wa 1985 na hata ukaimarika zaidi baada ya kuanzishwa kwa elimu bila malipo katika shule za msingi mwaka 2003. Ngugi (2009) akimnukuu Mbaabu (1996:131) anasema kuwa baada ya kutekelezwa kwa mfumo wa 8-4-4 vitabu vya watoto vilianza kuchapishwa kwa wingi. Hii ni kwa

sababu Kiswahili kilianza kuwa somo la lazima na linalotahiniwa katika shule za msingi na hivyo basi mahitaji ya vitabu vya hadithi za Kiswahili kuongezeka. Kuanzishwa kwa elimu ya dezo katika shule za msingi kumefanya wanafunzi wengi wasome vitabu vya hadithi za watoto kwa vile serikali ilianza kuzipatia shule pesa za kununulia vitabu vikiwemo vitabu vya hadithi (Ngugi 2009).

Uchapishaji wa hadithi za watoto ulipiga hatua kubwa shule zilipoanza kununua vitabu vya hadithi kwa wingi kuliko hapo awali. Wachapishaji mbalimbali walizindua miradi ya kuchapisha vitabu vya fasihi ya watoto ili kutosheleza mahitaji ya shule. Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu (2015), miongoni mwa wachapishaji kama hao ni Jomo Kenyatta Foundation (Wakfu wa Jomo Kenyatta) ambao walianza mfululizo wa hadithi za *Adili*, Kenya Literature Bureau (Shirika la Uchapishaji Kenya) ambao walianza mfululizo wa hadithi za *Nasaha Zetu*, Phoenix, OUP. Sasa Sema (Longhorn), EAEP, Moran, Vide-Muwa. Mashirika haya ya uchapishaji yamechangia pakubwa katika ukuaji na uenezaji wa fasihi ya watoto.

Ubora wa vitabu vya fasihi ya watoto vinavyochapishwa umeimarika miaka ya hivi karibuni. Ngugi (2009) anasema kuwa Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa (KICD) imechangia ubora huu kwa kuwa inakagua ufaafu wa vitabu vinavyochapishwa ili kuidhinisha vile vinavyofaa kusomwa na watoto shuleni. Jambo hili linafanya waandishi na wachapishaji kujitahidi kutimiza viwango vya ubora vinavyowekwa na taasisi hiyo. Kadhalika kumekuwa na mashindano mbalimbali ya waandishi kuwania zawadi ambayo yanawahamasisha waandishi kuandika hadithi bora za watoto. Mashindano kama hayo ni Tuzo ya fasihi ya Jomo Kenyatta na Tuzo ya Uandishi ya Wahome Mutahi.

Mbali na maendeleo katika uandishi na usambazaji wa vitabu vya hadithi za watoto, wasomi kadhaa wameshughulikia uhakiki wa fasihi ya watoto ya Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni. Miongoni mwao ni Mpesha (1996), Karuga (2005), Muthubi (2005), Kairu (2005), Matundura (2007) Ngugi (2009). Tafiti hizi zitaendelea kuimarisha ubora wa vitabu vya hadithi za watoto vinavyoandikwa hasa na wasomi waliosoma tasnifu za tafiti husika. Licha ya kwamba kuna juhudi nyingi zilizofanywa kuendeleza fasihi ya watoto, kuna haja ya kuendelea kuiimarisha zaidi kwa kuendelea kuifanyia uhakiki mara kwa mara kwa kuwa mabadiliko huendelea kutokea katika fasihi jinsi jamii inavyoendelea.

## 2.2 SIFA BAINIFU ZA HADITHI ZA WATOTO

Hadithi za watoto, ambazo ni kategoria ya fasihi ya watoto, ni hadithi zilizoandikwa huku walengwa wake wakuu wakiwa ni watoto. Hadhira kubwa ya hadithi hizi ni watoto ambao wako katika shule za msingi. Hadithi za watoto, kama fasihi ya watoto ilivyo, huweza kubainika kutokana na sifa maalumu. Baadhi ya sifa hizo ni kama zifuatavyo:

Wahusika wakuu wa hadithi za watoto huwa ni watoto. Wamitila (2002) anaeleza kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Wahusika huwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayosema na wanayoyatenda. Ingawa hadithi za watoto zinaweza kuhusisha wahusika wa aina mbalimbali kama vile wanyama na watu wazima, pengine wakiwa wazazi au walimu wa watoto wahusika, wahusika wakuu aghalabu huwa watoto. Hali hii hufanya kazi ishawishi mtoto kuisoma kwa kuwa atatamani kujihusisha na

mhusika huyo katika msuko wa hadithi nzima hasa iwapo mhusika yule ni shujaa na mwenye maadili. Endapo ni wahusika wanyama waliotumiwa, wao huonyeshwa wakitenda vitendo vya watoto au watu ambao watoto hutagusana nao katika mazingira yao ya kawaida. Katika utafiti huu tulizingatia hadithi zenye wahusika wakuu watoto ili kupata usawiri wa watoto. Kwa mfano, Juma na Maria katika *Mwepesi wa Kusahau* na Kerubo na Otambo katika *Likizo ya Mkosi*. Kuwepo kwa wahusika wakuu watoto kunachangia mtazamo unaotawala kazi husika kuwa wa watoto. Sifa hii hufanya watoto wanaosoma hadithi kuvutiwa na hata kujilinganisha na wahusika wenyewe. Hadithi za watoto mara nyingi huwa na mhusika mwema na mhusika mbaya ili watoto waweze kupata funzo linalokusudiwa. Kwa mfano katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* Maria amechorwa kama mhusika mwema ilhali Juma amechorwa kama mhusika mwovu. Katika hali hii watoto wanaosoma huona wema ukishinda uovu na hapo huwa wameelekezwa kimaadili.

Hadithi za watoto huwa fupi na za kiutendaji. Hii ni kwa sababu hadithi ikiwa ndefu itawachosha watoto wanaosoma na watakosa hamu ya kuisoma na kuimaliza. Hadithi zilizoteuliwa katika utafiti huu zina kurasa kati ya arubaini na hamsini.

Lugha katika hadithi za watoto huwa nyepesi kulingana na kiwango cha watoto wanaolengwa ili mtoto msomaji aweze kuifuata hadithi, kuifurahia na kupata ujumbe wake. Mathalani, hadithi zinazolenga watoto wa madarasa ya chini katika shule za msingi zina lugha nyepesi kuliko vitabu vya hadithi zinazolenga watoto wa madarasa ya juu. Sentensi mara nyingi huwa fupi na zenye miundo sahili ili ujumbe uweze kueleweka wazi na bila utata kwa kuwa urazini wa wasomaji chipukizi huwa mdogo. Msamiati unaotumika huwa na wepesi unaolingana na kiwango cha watoto

wanaolengwa. Lugha ngumu inaweza kuathiri uelewekaji wa hadithi na watoto wanaosoma. Katika hadithi zote mbili zilizoteuliwa katika utafiti huu, mwandishi ametumia lugha ambayo mtoto anaweza kuelewa. Lugha imejikita katika kiwango cha mtoto kwa upande wa msamiati, aina na miundo ya sentensi na ujumbe kwa jumla. Mathalani, hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* ambayo inanuiwa watoto wa darasa la nne ina lugha nyepesi kidogo kuliko ya *Likizo ya Mkosi* ambayo inalenga watoto wa darasa la sita.

Hadithi za watoto huwa na picha au michoro ya kuvutia aghalabu yenye rangi mwafaka. Picha hizi huvutia watoto kusoma hadithi, husaidia weledi wao, huwawezesha kukumbuka hadithi wakiisoma na pia hupatia hadithi uhalisia. Picha na michoro ni njia muhimu ya kupitisha ujumbe katika hadithi za watoto. Picha huwa zinalingana na ujumbe unaopitishwa. Mathalani, picha katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* zinamsawiri Juma kama mvulana mchafu, asiyejali na anayebaki nyuma (tazama kiambatisho B).

Maandishi ya hadithi za watoto huwa na ukubwa unaolingana na kiwango cha watoto wanaolengwa. Kazi za watoto wa madarasa ya chini, ambao ndio wanaanza kujifunza kusoma, huwa na maandishi makubwa sana ili kumwezesha mtoto atambue herufi haraka na kuweza kusoma. Zile za watoto wa madarasa ya kati pia huwa na maandishi makubwa kiasi kuliko zile za watoto wa madarasa ya juu katika shule za msingi. Kwa mfano, Kitabu cha *Mwepesi wa Kusahau* ambacho kinakusudiwa wototo wa darasa la nne kina maandishi makubwa kuliko cha *Likizo ya Mkosi* ambacho kinakusudiwa watoto wa darasa la sita.

Msuko wa hadithi za watoto huwa mwepesi na wa moja kwa moja. Kwa mfano, mbinu rejeshi huepukwa ili wasomaji wa umri mdogo wanaolengwa waweze kufuata kisa kwa wepesi kutoka mwanzo, kilele hadi mwisho. Sifa hizi humwezesha mtoto anayesoma kufuata matukio yenyewe na kuelewa bila kuchanganyikiwa wala kuchoka. Kitabu kizuri cha mtoto ni kile ambacho mwandishi amefaulu kuwasiliana moja kwa moja na mtoto anayelengwa. Katika hadithi za utafiti huu mtiririko ni wa moja kwa moja kwa kuwa mwandishi ametumia tukio, sababisho lake na matokeo katika hadithi zote mbili.

Maudhui ya hadithi za watoto huwalenga watoto. Wamitila (2002) anaeleza maudhui kama jumla ya masuala na mambo yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Waandishi wa hadithi za watoto hujikita katika ulimwengu wa mtoto na kazi zao huhusu tajriba za watoto kama vile majukumu yao katika jamii, maadili na shughuli zao shuleni na nyumbani. Huwa na mada au wazo kuu linalolenga na linalowavutia watoto. Kwa mfano hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* inakemea uzembe na tabia ya kusahausahau huku ikisifu bidii na usafi. *Likizo ya Mkosi* nayo pia inahimiza maadili na ushirikiano mbali na bidii. Maudhui ya hadithi hizi ni rahisi kueleweka na watoto. Dhamira kuu pia huhusu watoto. Dhamira hii hukusudiwa kuwa funzo kwa watoto.

Mandhari ya hadithi za watoto aghalabu huwa ni mazingira ambayo yanahusishwa na shughuli au matendo ya watoto na maisha yao ili watoto halisi wanaosoma hadithi husika waweze kujitambulisha nazo. Mazingira haya ni kama vile shuleni, nyumbani, porini uwanjani na njiani. Kwa mfano, katika hadithi zote mbili tulizochunguza, matukio yanafanyika katika mandhari ambayo ni mazingira ya kawaida ya watoto. Watoto mara nyingi huwa katika shughuli za nyumbani au za shuleni. Matukio mengi

katika hadithi hizi mbili yanatokea katika mandhari ya nyumbani au shuleni. Kwa mfano, mwanzoni mwa hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* tunakutana na Juma na Maria wakiwa nyumbani katika shughuli za kujitayarisha ili waende shuleni kisha mwishoni tunawaona watoto hao shuleni ambako wamejumuika na watoto wengine kwenye paredi. Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* Kerubo na Otambo mara nyingi wako katika mandhari ya nyumbani. Walikuwa ama nyumbani kwao au nyumbani kwa nyanya yao ambako wanashughulika katika shughuli za nyumbani kama vile kupika na pia shughuli za shambani kama vile kuvuna. Haya ni mandhari yanayofahamika kwa urahisi na watoto. Majina ya watoto hawa pia yanawakilisha jamii maana ni majina yanayofanana na yale yanayopewa watoto halisi katika mandhari yanayotambulikana kijamii.

Hadithi za watoto huegemea fantasia. Sifa hii inamaanisha kuwa huwepo mambo mengi ya ajabuajabu ambayo kwa kawaida hayatokei katika maisha ya kila siku. Wamitila (2003) anasema kuwa ni matukio yanayokiuka uhalisia na tajriba ya watoto na ambayo ni msingi mkubwa katika fasihi hii inayokiuka ulimwengu wa kijarabati na kuingia kwenye ulimwengu wa kimazingaombwe na ndoto. Sifa za kimaajabu ni kawaida katika fasihi ya watoto. Fantasia hufanya kazi hizi ziwafurahishe watoto kwa kuwa huwatoa katika ulimwengu wa kawaida. Kwa mfano, katika hadithi nyingine ya Matundura (2013) *Hazina ya Zuena na Makombo*, kuna kijibwa kilichojitokeza kiajabu. Watoto wawili waitwao Zuena na Makombo walikuwa wamekubaliana kutumia hazina yao kununua mbwa. Waliondoka nyumbani kwenda sokoni kutafuta mnyama huyo. Huko sokoni walivutiwa na vitu vingine na wakavinunua. Pesa walizokuwa nazo ziliisha kabla hawajanunua mbwa. Walipokuwa wanarudi nyumbani

bila mbwa, Zuena na Makombo walishangaa kuona kijibwa cheusi kikiwa nyuma yao. Walikichukua kwenda kukitunza.

Mvuto na upokezi wa watoto wa hadithi ni sifa muhimu sana katika hadithi za watoto ili kujenga ilhamu ya kupenda kusoma hadithi hadi mwisho. Wamitila (2002) anaeleza mvuto kuwa ni hisia alizonazo msomaji kumhusu mhusika fulani. Kwa kawaida Ikiwa msomaji amevutiwa na mhusika fulani atapatwa na hamu ya kutaka kujua yatakayompata. Dhana ya mvuto katika hadithi inahusisha vipengele vingi. Kazi hiyo sharti iwe na mtazamo wa watoto. Watoto hufikiria kwa njia tofauti na watu wazima na si lazima wafurahishwe na mambo yanayowafurahisha watu wazima. Wao basi hutekwa na kazi iliyoandikwa kwa matarajio na matamanio yao kulingana na wakati wanamoishi. Mvuto mkubwa katika fasihi ya watoto hutokana na uwezo na nguvu yake ya usimulizi. Usimulizi huu unajifunga katika maelezo ya mambo ambayo ni muhimu tu katika kuijenga hadithi.

Watoto huvutiwa na hadithi zenye tendo la ujasiri pamoja na mapambano yanayotokea. Wamitila (2008) anasema kuwa mhimili mkubwa katika fasihi ya watoto ni tendo kuu, jasira na usimulizi wa jasira hiyo pamoja na mapambano yanayotokea. Wamitila anaeleza kuwa jasira ni tukio fulani la uvumbuzi na ambalo linaweza kuhusishwa na safari inayokumbwa na matatizo. Usimulizi mwingi wa hadithi uanajengwa kwenye maelezo ya jinsi mhusika mkuu anavyokabili vikwazo njiani na hatimaye kuishia kufanikiwa kwa mfano katika safari ya kutoka kwenye msitu fulani, uwindaji msituni, maisha bila wazazi au changamoto shuleni. Katika *Mwepesi wa Kusahau*, kwa mfano, Juma anatembea safari ndefu ya maisha huku akikabiliana na changamoto nyingi zinazotokana na ujana na hatimaye anaamua

kubadilika na kuwa mwema. Katika *Likizo ya Mkosi*, Kerubo na Otambo wanatamani sana kwenda katika burudani na utulivu wa likizo. Wanafanya mengi kukabiliana na vikwazo vilivyokuweko kama vile kujitahidi wapate matokeo bora masomoni ili baba yao akubali kuwapa ruhusa ya kwenda kutembea na pia kutafuta zawadi zilizowafaa nyanya na babu. Hatimaye wanafanikiwa kwenda kwa nyanya yao kama walivyotamani lakini likizo yao inaishia kukumbwa na mkosi baba yao anapohusika katika ajali ya barabarani na ikawalazimu watoto hao kukatiza likizo yao.

Hadithi zilizoandikiwa watoto huwa na taharuki. Watoto wanaposoma hadithi huwa na hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusu yatakayotokea mwishoni. Waandishi wa hadithi za watoto huhusisha wahusika wanaotaka kupata kitu fulani lakini wanaokabiliwa na vikwazo mbalimbali. Sifa hii tunaiona kwa mfano katika *Likizo ya Mkosi* wakati watoto wanataka kwenda kwa nyanya yao lakini wanatakiwa na baba yao kwanza wapate matokeo mazuri shuleni muhula huo. Pia, Juma anapokimbizwa na mwalimu Madenge katika *Mwepesi wa Kusahau,* mbio zao zinasababisha taharuki kubwa miongoni mwa watoto wanaosoma kisa kile ili waone mbio za sakafuni zitakavyoishia ukingoni. Hali hii ya taharuki humpa mtoto hamu ya kusoma ili ajue hadithi itakavyoishia.

Mwanzo na mwisho wa hadithi hizi kwa kawaida huibua hisia za burudani. Funzo kuu la hadithi hujitokeza kwa urahisi mwanzoni au mwishoni mwa hadithi huku likimshajiisha mtoto msomaji na kujenga uadilifu ndani yake. Watoto huvutiwa na hadithi zinazoathiri hisia na matarajio yao katika jamii wanamoishi.

Kisa katika hadithi za watoto aghalabu huchukua kipindi kifupi kiwakati. Kwa mfano, katika *Mwepesi wa Kusahau* kisirani kinachomkumba Juma kutokana na mwenendo wake mbaya kinatokea siku moja ya Ijumaa. Vilevile kisa kikuu cha *Likizo ya Mkosi* kimefanyika katika kipindi cha likizo moja.

## 2.3 DHIMA YA HADITHI ZA WATOTO

Hadithi za watoto si maandishi ya vichekesho na vituko visivyo na uhusiano na maisha ya kawaida katika jamii. Hadithi hizi hubuniwa kutokana na mambo halisi yanayoendelea katika jamii zikilenga kuifahamisha jamii mambo yaliyo mazuri na yale mabaya. Tukio na mandhari huwa ya kweli au yenye uhusiano na hali halisi ya ulimwengu unaomzunguka mtoto. Hivyo basi, hadithi za watoto ni sanaa inayoelezea maisha ya watoto kwa njia bunifu inayojikita katika msingi na kaida zinazotawala maisha halisi ya jamii kisosholojia.

Kama fasihi nyingine, lengo kuu la hadithi za watoto ni kuburudisha. Watoto husoma kama njia ya kujistarehesha. Warren na Wellek (1973) wanaeleza kuburudisha huku kama kuburudisha kwenye udhati kwa kuwa burudani ya kazi ya kifasihi ni burudani inayoelimisha. Maudhui ya hadithi pamoja na fani zilizotumiwa huibua hisia za burudani na kustarehesha. Wandishi hutumia lugha teule inayogusa hisia za mtoto anayesoma na kumfanya ahisi kutosheka au kuridhika anapoisoma ile hadithi. Picha na michoro iliyomo huweza kuchangamsha na kuleta burudani wakati wa kusoma. Kwa mfano, picha ya jalada katika *Mwepesi wa Kusahau* ambapo pana watoto wawili wanaofukuzana kwenda shule mmoja akiwa safi na mwingine mchafu huenda ikaibua

hisia za ucheshi miongoni mwa watoto na kuwavutia kusoma ile hadithi (tazama kiambatisho B).

Mbali na burudani hadithi za watoto zina dhima ya kuelimisha. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuelimisha huku hutokana na yanayosimuliwa kwenye hadithi. Hadithi za watoto basi hujenga hulka za watoto na kuwafanya wapate mafunzo yanayojenga maadili yao. Hadithi huweza kuwaongoza watoto kufanya uamuzi wa maana na kuweza hukata shauri kuhusu ukweli na ubora wa yale wanayosoma katika hadithi.

Hadithi zote mbili tulizochunguza katika utafiti huu zina thamani za kimaadili kama vile kuonya, kukanya na kutahadharisha ili kuwajenga watoto wakutegemewa na jamii kwa vile watoto wanaozisoma wanaweza kutazama maisha yao kupitia kwa wahusika watoto wa hadithini. Kwa mfano, hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* inaweza kumtahadharisha mtoto mwenye mwenendo mbaya kama ule wa Juma na kumfanya abadili tabia na kuwa mwaadilifu kama Maria. Hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* inasifu tabia njema kama vile usafi, kufika shuleni kwa wakati unaofaa na kufanya bidii masomoni. Ile ya *Likizo ya Mkosi* ina mafunzo kama vile uwajibikaji na bidii kati ya mengine ambayo yanaweza kumshawishi mtoto anayesoma kuwa na bidii, kujitolea na kuwajibika daima kama vile Kerubo na hata ndugu yake Otambo walivyojitahidi kufanya.

Hadithi za watoto huwaelimisha na kuwafunza jinsi ya kukabiliana na matatizo ya ulimwengu au ya jamii. Mwandishi wa hadithi huweza kuelimisha ama kimakusudi au kisadfa kutokana na maudhui yaliyomo. Licha ya hayo, mtoto shuleni anaposoma hadithi ataweza kupata mawazo atakayoweza kutumia anapoandika insha na hivyo

kukuza ubunifu wake. Vitabu vya hadithi za watoto huwakuza kimawazo na kuchochea fikira za ubunifu miongoni mwao huku vikiwapa hamu ya kutaka kujua mengi.

Watoto hukuza lugha na kujenga msamiati wanaposoma hadithi. Kwa hakika, katika shule za msingi ni muhimu watoto kusoma vitabu vya hadithi ili waweze kujenga lugha watakayotumia katika uandishi wao wa insha. Usomaji wa vitabu vya hadithi utawasaidia kujiimarisha kisarufi, kimsamiati na kujifunza uakifishaji ili kukuza uwezo wao wa kuandika.

Hadithi za watoto aghalabu huangazia masuala ibuka yanayoikabili jamii na wakati mwingine hutoa suluhisho. Hivyo basi watoto wanapozisoma hupata ufafanuzi wa masuala yanayowatatiza katika maisha yao. Hadithi hizi hutuchorea taswira ya uhalisi wa maisha ya jamii kwa njia ya ubunifu. Hivyo hadithi huwasilisha hali, maingiliano na mivutano miongoni mwa watu na mazingira yao. Hili hufanyika kutokana na jinsi wahusika katika hadithi walivyosawiriwa. Kwa mfano, hadithi tulizopitia hatika utafiti wetu zilibainisha tofauti katika usawiri wa mtoto wa kike na wa kiume katika jamii. Huenda mwandishi alikuwa na nia ya kuhamasisha jamii kuendelea kumthamini mtoto wa kike.

Kwa jumla hadithi za watoto huathiri hisia na matarajio yao katika jamii wanamoishi. Usawiri wa wahusika watoto unaweza kuathiri uamuzi watakaotoa watoto wanaosoma vitabu vya hadithi. Hii ni kwa sababu wanapokea ujumbe wanaoandikiwa na wanaweza kukumbuka kwa urahisi yale waliyosoma hasa ikiwa ujumbe huo una ukweli fulani kuhusu maisha yao katika jamii. Hivyo ipo haja ya kuhakiki vitabu vya

hadithi za watoto ili kuhakikisha kwamba watoto watasoma yale yanayofaa kwa ajili ya kuwajenga kimaadili na kuwapa mielekeo inayofaa katika jamii ili jamii iwe na vizazi bora vya siku za usoni.

## 2.4 HITIMISHO

Katika sehemu hii tumejadili sifa za hadithi za watoto. Kutokana na utafiti huu imebainika kuwa hadithi za watoto zina sifa maalumu ambazo zinazitambulisha. Sifa hizo zinahusisha dhana kadhaa zikiwemo wahusika watoto, ufupi, lugha nyepesi, picha, ukubwa wa maandishi, msuko mwepesi, maudhui yanayolenga watoto, fantasia, mvuto, taharuki na mwisho wa kusisimua. Tumejadili pia majukumu ya hadithi za watoto katika jamii ya sasa. Tumeona kuwa majukumu ya fasihi ya watoto na yale ya fasihi ya watu wazima yana uhusiano na ni kama vile kuburudisha, kuadilisha, kuelimisha, kukuza lugha, kuchochea fikira na hata kuangazia masuala yanayoibuka katika jamii.

# SURA YA TATU

## USAWIRI WA WATOTO KATIKA *MWEPESI WA KUSAHAU*

### 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tumejadili usawiri wa watoto katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau*. Tumeanza kwa kutoa muhtasari wa hadithi yenyewe kisha tukaangazia taswira zinazobainika za mtoto wa kike na zile za mtoto wa kiume. Baadaye tumelinganisha usawiri wa watoto wa kike na wale wa kiume ili kuona ikiwa kuna wale wanaosawiriwa kwa njia chanya kuliko wengine. Tumetamatisha sehemu hii kwa kujadili mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume.

### 3.1 MUHTASARI WA *MWEPESI WA KUSAHAU*

*Mwepesi wa Kusahau* ni hadithi iliyo na wahusika wawili wakuu ambao ni Juma na Maria. Juma ni mvulana na Maria ni msichana. Juma na Maria walikuwa mapacha waliofanana kama shilingi kwa ya pili. Wazazi wao walikuwa wameajiriwa kazi za serikali, mama akiwa muuguzi mkuu na baba yao akiwa tabibu wa mifugo. Wazazi hao walijitahidi kuwapa malezi bora na kuwaelimisha watoto wao wawili wakiamini kuwa elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Watoto hao wawili walinunuliwa mahitaji yao yote ya shule. Wote walikuwa darasa la nne katika shule ya msingi ya Jengahekima.

Ingawa wote walipenda kwenda shule, Juma alikuwa na matatizo mengi. Alikuwa hatilii masomo maanani na alikuwa na tabia ya kusahau haraka mambo mbalimbali aliyoambiwa afanye. Kwa upande wake, Maria alimakinika masomoni, alikuwa mwerevu, alizingatia usafi na alikuwa mwenye bidii na asiyesahau mambo. Walimu

na wazazi wake walimpenda. Maria alikuwa mwenye kuwajibika ilhali ndugu yake Juma alikuwa mtepetevu. Tofauti katika tabia za wawili hawa zinaanza kudhihirika katika ukurasa wa 16 tunapoambiwa hivi:

> Ijumaa moja, Maria aliamka mara moja alipowasikia jogoo wakiwika … alimwangalia ndugu yake Juma, aliyekuwa amelala kwenye kitanda kando na chake. Juma alikuwa amelala fo fo fo. Licha ya kuwa mwepesi wa kusahau, Juma pia alikuwa mzito wa usingizi. Hakusikia kamwe jogoo wakiwika. (Uk 16)

Ilikuwa Ijumaa siku ya kwenda shule lakini Juma aliendelea kulala licha ya jogoo kuwika. Maria alijaribu kumwamsha lakini Juma hakutoka kitandani hata alipoamshwa. Mwishowe Juma aliamka akiwa amechelewa, Maria aliondoka kwenda shuleni huku akimwaacha nyuma Juma. Hata alipoamka, Juma alipoteza wakati zaidi nyumbani huku akiitafuta kalamu yake. Alikuwa amesahau kuwa alikuwa ameidunga kwenye shungi lake la nywele hadi mama yake alipomzindua. Hatimaye alifika shuleni akiwa amechelewa kwa sababu ya kutoamka na kujiandaa mapema.

Kwa sababu ya kufika shuleni akiwa amechelewa, Juma anaamua kujificha nyuma ya ua ya shule. Mwalimu wake alimwona na kumuita lakini Juma hakutii. Juma alitoroka naye mwalimu akakimbizana naye hadi akamshika na kumpeleka shuleni. Wanafunzi waliokuwa kwenye gwaride la asubuhi wakingojea kukaguliwa usafi walimwangalia Juma kwa mshangao mkubwa. Walinong'onezana huku wakiwa hawamini waliyoyaona. Sare ya Juma ilikuwa imelowa kutokana na umande wa nyasi, shati lake jeupe lilikuwa na madoadoa ya damu kutokana na kuumwa na siafu waliokuwa pale alipokuwa amejificha. Nywele zake hazikuwa zimechanwa. Viatu vyake vilikuwa havijapakwa rangi. Hakupendeza hata kidogo. Macho ya wanafunzi yalimgeukia Maria, ambaye alikuwa mtanashati, kama kwamba wanafunzi hao walikuwa wakiwalinganisha mapacha hao. Baadaye, mwalimu wao alimwambia

Maria awashauri wanafunzi wote akiwemo Juma juu ya umuhimu wa usafi. Kisirani kilichomkumba Juma siku hiyo kilikuwa adhabu ya kutosha. Kutoka siku hiyo aliamua kuiga tabia nzuri ya dada yake, Maria.

Mwandishi anawafunza watoto kwamba wanapaswa kuepuka tabia mbaya kama za Juma na kuwajibika kama Maria. Mambo ambayo mwandishi ameshughulikia katika hadithi hii ni ya kuaminika na kuna uwezekano baadhi ya watoto wenye umri kama wa Juma na Maria watachangamshwa na vituko vinavyofanyika kwa sababu huenda wameshuhudia mambo sawa na hayo katika mazingira yao. Wengine waweza kuwa na tabia kama ya Juma wakawa ni wavivu, wepesi wa kusahau, wachafu na wasiochana nywele. Watoto pia wanaweza kuhusisha Juma na watoto wengine wanaowajua shuleni mwao. Kwa hivyo tunaweza kuyatathmini matukio katika hadithi hii kwa mtazamo wa sosholojia ya fasihi.

## 3.2 TASWIRA ZINAZOBAINIKA ZA MTOTO WA KIKE

Njogu na Chimerah (1999: 33) wanasema taswira ni mkusanyiko wa picha anazopata msomaji baada ya kusoma kazi ya fasihi. Hivyo taswira ni dhana inayotumiwa katika uhakiki wa fasihi kwa maana ya mkusanyiko wa picha zinazoundwa akilini kutokana na maelezo ya msanii katika kazi yake. Katika utafiti wetu tulichunguza taswira chanya na hasi za mtoto wa kike na wa kiume zinazobainika katika hadithi za watoto za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*.

Katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* dhana ya mtoto wa kike inawalikishwa na mhusika Maria. Msichana katika hadithi hii amesawiriwa akiwa na sifa nyingi chanya. Msichana amechorwa kama mtu mwenye bidii, makini katika masomo,

mwerevu, safi, mtoto aliyependwa na wazazi pamoja na walimu wake na mwenye kukumbuka mambo. Katika ukurasa wa 9 mwandishi anasema hivi kumhusu Maria:

> Maria alikuwa mwanafunzi makini, safi na mwenye bidii za mchwa masomoni. Hakusau jambo lolote kwa urahisi. Walimu na wazazi wake walimpenda mno kwa kutosahau. Wanafunzi wenzake walimtania kuwa akili zake zilinasa kila kitu kama vile sumaku inasavyo wembe. Maria alikuwa mwerevu. (Uk 9)

Msichana pia amesawiriwa kama mwenye kuiga mambo mazuri ya watu. Katika ukurasa wa 10 tunaelezwa kuwa:

> Maria aliiga kila jambo zuri kutoka kwa wazazi wake, walimu na wanafunzi wenzake. Hata hivyo alijihadhari sana kuiga mambo mabaya. (Uk 10)

Tabia moja nzuri aliyokuwa ameiga ni ile ya kuandika maagizo kwenye shajara ili asije akayasahau. Tabia hii alikuwa ameiiga kutoka kwa baba yake, Hamisi Akida. Baba yake alikuwa na tabia ya kuandika kumbukumbu zake za kazi yake ya kutibu mifugo kwenye shajara ili akumbuke siku ya kufanya kila kazi yake asiwakosee wakulima wa mifugo.

Msichana amechorwa kama mwenye kuwajibika katika mambo aliyofanya. Kwa mfano, Maria anaamka mapema na kwenda shule bila kuchelewa huku ndugu yake Juma akiwa bado amelala.

Mtoto huyu wa kike amechorwa kama mtu mwenye mipango na aliyependa kusoma. Kwa mfano katika nukuu hii:

> Huku chai ikiendelea kupoa, Maria alitoa shajara yake kuangalia ni mipango na kazi ipi aliyotarajiwa kufanya siku hiyo ya ijumaa, tarehe 15 mwezi wa Machi. Aliona kuwa alifaa kumrudishia rafiki yake Angela kitabu chake, *Mkasa wa Shujaa Liyongo*, alichomwomba kusoma. Alikuwa amebakisha kurasa kumi hivi akamilishe hadithi kwenye kitabu hicho ambayo ilimvutia mno. (Uk 21)

Maria amesawiriwa kama aliyependa kusoma. Alipenda kusoma vitabu vya ziada. Kwa mfano tunamwona akisoma kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* alichokuwa amemwomba rafiki yake.

Maria alikuwa mshauri wa wanafunzi wenzake. Mwishoni mwa hadithi tunaelezewa kuwa:

> Maria alipatiwa nafasi ya kuieleza shule nzima siri ya ushindi wake. Bila kusita, Maria aliwadokezea wanafunzi wenzake umuhimu wa kutumia shajara kujikumbusha mambo yaliyokuwa wajibu wao. Wanafunzi wote waliapa kuuiga mfano wake. (Uk 43)

Hapa Maria anaonekana akiwashauri wanafunzi wenzake akiwemo Juma juu ya siri ya kuwa na mipango ili kufaulu. Hivyo tunaweza kusema kuwa mtoto wa kike ni mshauri wa wanafunzi wengine shuleni na mfano wa kuigwa.

Kwa kuwa Maria anasawiriwa kwa sifa ambazo zinaweza kuigwa na watoto. Wasichana wanaosoma hadithi hii wanaweza kuichangamkia na pengine kujinasibisha na Maria.

Usawiri huu wa msichana Maria, ni kielelezo cha taswira ya msichana miongoni mwa jamii zetu ambapo kuna madai kuwa msichana amempiku mvulana masomoni (tazama kiambatisho A). Miongoni mwa jamii zetu kuna dhana kuwa wasichana huzingatia usafi kuliko wavulana na ni wenye kujitunza na kutunza vitu vyote vinavyowahusu kama vile mavazi, vitabu na hata nyumba sawa na vile Maria alivyofanya. Kwa jumla wasichana huwajibika zaidi katika mambo mengi kwenye jamii.

### 3.3 TASWIRA ZINAZODHIHIRIKA ZA MTOTO WA KIUME

Mtoto wa kiume katika hadithi hii anawakilishwa na mhusika Juma. Kwa jumla, Juma amesawiriwa kama mwenye sifa nyingi hasi na tofauti kabisa na dada yake Maria. Amechorwa kama aliyekuwa na matatizo mengi. Matatizo yake yamkini ni kielelezo cha changamoto zinazowapata wavulana katika jamii ya sasa inayoelekea kujali maslahi ya mtoto wa kike zaidi kuliko yale ya mtoto wa kiume.

Mvulana huyu anasawiriwa kama msahaulifu (mwepesi wa kusahau) ambaye alisahau hata kalamu yake ilikuwa wapi ilihali alikuwa ameichomelea kwenye nywele zake mwenyewe. Mama yake anamkuta akitafuta kalamu na ndiye anayemzindua kwa maneno haya:

> "Waona jinsi uzembe na usahaulifu ulivyo mbaya? ... kalamu yako ipo kichwani mwako." (Uk 30)

Mvulana amesawiriwa kama mtu mzembe. Juma anaonekana mzito wa usingizi na anayependa kulala kwa kuwa anaamka kwenda shule wakati Maria alipokuwa anamaliza kunywa chai yake kama tunavyoona katika nukuu hii:

> Maria alipokuwa anamalizaia kunywa chai yake , ndipo Juma alipoamka. Ilikuwa saa mbili kasorobo. (Uk 22)

Mtoto wa kiume aonekana kama ni mwenye mapuuza. Kwa mfano, tunaelezewa kuwa:

> Juma alikuwa na matatizo mengi. Mosi, hakutilia masomo maanani. Pili, alikuwa na tabia ya kusahau haraka mambo mbalimbali aliyoambiwa afanye. Juma alikuwa mwepesi wa kusahau. (Uk 9)

Mvulana anayewakilishwa na mhusika Juma amechorwa kama mtoto asiyejali. Kwa mfano, Juma analala kifudifudi kwenye nyasi kichakani alikojifisha bila kujali umande uliokuwepo na bila kuona kwamba kulikuwa na siafu.

Bila kujali umande uliokuwa kwenye nyasi, Juma alilala kifudifudi. (Uk 34)

Mvulana anasawiriwa kama aliye mchafu. Kwa mfano katika mchoro wa jalada tunamwona Juma akiwa hakuchana nywele na alivalia ovyoovyo mavazi yake ya shule. (Tazama kiambatisho B)

Kwa hakika, katika michoro yote kwenye hadithi hii, Juma anaonekana akiwa mchafu na aliyejiachilia. Nywele yake haijachanwa, mavazi ni machafu na shati linaning'inia ovyo mwilini.

Shuleni, mvulana amesawiriwa kama mtundu. Kwa mfano, mwalimu wake alipomuita Juma atoke alikokuwa amejificha hakumtii. Badala yake alitoroka na ikambidi mwalimu amkimbize.

Juma alijifanya kutosikia na kukimbia kadiri miguu yake ilivyoweza. (Uk 37)

Mwalimu alipomkamata alimpeleka mbele ya paredi shuleni akiwa mchafu. Kitendo hiki cha mwalimu kinamwaibisha Juma mbele ya wanafunzi wenzake na kumsawiri kama aliye tofauti kabisa na Maria ambaye alikuwa mwenye nidhamu. Kwa hakika, anaonekana kama anayemwaibisha dada yake ambaye amesawiriwa kama nadhifu na mtiifu.

Nyumbani, mama naye haonekani kumjali sana huyu mtoto wa kiume. Kwa mfano, Maria anapojitokeza kupata kiamsha kinywa mazungumzo kati ya mama na Maria kumhusu Juma yanaendelea hivi:

> "Juma yuko wapi?" Mama alimkata usemi (Maria)."Nimemwamsha akakataa katakata kuamka. Amelala na kukoroma mithili ya chura," Maria alisema huku akimwangalia mama yake aliyekuwa kavaa tabasamu usoni. "Mwepesi wa kusahau, hajui kwamba leo ni Ijumaa? Mwache achelewe shuleni apate adhabu," Mama alisema huku akimpisha Maria...(Uk 19 – 20)

Kule kutopenda shule kwa Juma kunadhihirisha tabia ya baadhi ya wavulana katika jamii wasiopenda kwenda shuleni. Mambo ambayo Juma anatenda kama vile kulala hadi akachelewa na shule, kutochana nywele na kuvaa shati lake likiwa limening'inia ovyo ni tabia ambazo zinapatikana miongoni mwa baadhi ya wavulana shuleni.

Mhusika huyu amesawiriwa kama aliyepotoka. Watoto wanaposoma kuhusu Juma wanaweza kumlinganisha na baadhi ya watoto kama yeye wanaowajua shuleni na hata nyumbani. Watoto wanaweza wakaelewa athari za vitendo vibaya kutokana na aibu inayompata Juma na huenda jambo hilo likwa funzo kwa wale ambao wana tabia kama hizo.

Matukio kama haya yakimulikwa kwa nadharia ya sosholojia ya fasihi yanaakisi hali inayowakumba baadhi ya wavulana shuleni na nyumbani. Kwa mfano, katika jamii zetu hupatikana visa ambapo wavulana waweza kuwa wana vyumba vyao vya kulala ambayo vimetengwa na ile nyumba kuu ya wazazi na wavulana hao wakawa wanaishi humo vyumbani bila ya wazazi kuingia ndani kujua ni yapi huwa yanaendelea humo. Hivyo basi mvulana kama huyo aweza kuchelewa kwenda shuleni kwa sababu alilala

kupita kiasi akiwa chumbani mwake bila mzazi kumwamsha. Chumba hicho pia chaweza kukaa bila kusafishwa na kikawa kichafu kama kile cha Juma. Juma basi aweza kuchukuliwa kuwa kielelezo cha hali inayowakumba baadhi ya wavulana katika jamii ambapo hawapati watu wanaojali maslahi yao kwa dhati shuleni na hata nyumbani. Anwani ya kitabu hiki inatokana na tabia ya Juma ya kuwa mwepesi wa kusahau.

### 3.4 ULINGANISHI WA USAWIRI WA WATOTO WA KIKE NA WA KIUME KATIKA *MWEPESI WA KUSAHAU*

Juma na Maria walikuwa darasa la nne katika shule ya msingi. Kwa hivyo tunaweza kukisia ni watoto wa miaka kumi hivi tukiwalinganisha na watoto katika maisha ya kawaida. Ingawa walikuwa katika daraja moja shuleni, wamesawiriwa kwa njia tofauti kabisa kitabia. Mwandishi ametumia mbinu ya ukinzani ili kuweza kutofautisha wahusika hawa wawili mmoja akisawiriwa kama mwaadilifu na yule mwingine kama mwenye tabia mbaya. Jambo hili huenda likamwezesha mtoto anayesoma hadithi hii kujinasibisha na mhusika mwema.

Mtoto wa kike anasawiriwa kwa njia chanya zaidi kuliko mtoto wa kiume. Mtoto wa kike, Maria, anasawiriwa kama mwenye kuwajibika katika shughuli zake zote nyumbani na shuleni ilhali Juma, ambaye ni mtoto wa kiume, anasawiriwa kama mtu asiyejali akiwa nyumbani na hata shuleni.

Maria amechorwa kama aliyemakinika masomoni, mwerevu, mwenye bidii, mtiifu na anayekumbuka mambo haraka. Kinyume na sifa hizi, nduguye hajamakinika masomoni, ni mvivu, mtundu na mwepesi wa kusahau. Maria anafika shuleni kwa wakati ilhali Juma anachelewa kufika. Tabia ya Juma ya kusahau inasababisha

kuchelewa kwake kwa sababu alisahau alikoiweka kalamu na akachukua muda mrefu sana kuitafuta hadi mama yake alipomkumbusha kuwa aliichomelea kalamu nyweleni mwake.

Kuhusu uhusiano wake na wengine, Maria ni mtoto aliyependwa na wazazi pamoja na walimu wake, ni mshauri wa wanafunzi wengine shuleni na mfano wa kuigwa. Juma kwa upande wake haelekei kupendwa na yeyote wala hawezi kuwashauri wengine kwa vile amesawiriwa kama mwenye hasira na mwana mpotevu.

Michoro iliyo katika hadithi hii kuanzia kwenye jalada inashadidia tofauti hii kubwa kati ya usawiri wa mvulana na msichana. Katika michoro yote kwenye kitabu hiki msichana amechorwa akiwa nadhifu ilhali mvulana ni mchafu na mwenye nywele na nguo ambazo zimeachiliwa kukaa ovyoovyo.

Hadithi hii inamsawiri msichana akiwa mwenye mipango kuliko mvulana. Mathalani, katika picha ya jalada (tazama kiambatisho B) vitabu vya Maria vimo mkobani ilhali vya Juma vinatawanyika chini. Maria tayari amevalia sare yake vizuri kinyume na Juma ambaye anajaribu kuivaa ovyoovyo na haonekani nadhifu. Maria daima anaonekana akiwa mwenye kudumisha usafi na kuiga mambo mazuri ya watu wakati ambapo Juma ni mchafu. Juma hachani nywele zake wala kupanga vitu vyake vizuri. Mwishoni mwa hadithi Maria anatuzwa ilhali Juma anaadhibiwa.

Kwa kuwa fasihi ni kioo cha jamii, matukio katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* yaelekea ni kielelezo cha yale yanayopatikana miongoni mwa jamii. Katika jamii ni kawaida watoto wazuri kama Maria kutuzwa na wale wenye tabia mbaya kama Juma

kuadhibiwa. Hadithi hii ni yenye uhalisia na inaakisi maisha ambayo watoto waweza kuyatambua. Mpesha (1996) anasema kuwa hadithi zinazojikita katika usawiri wa maisha kama yalivyo zinakubalika na kupokewa zaidi na watoto kwa sababu wao huona ukweli wa mambo wanayoshuhudia au kuyafanya utotoni mwao na hivyo huweza kuyafahamu haraka na kuyachangamkia.

Hadithi za watoto, kama ilivyo fasihi, ni kazi za kibunifu zilizo na jukumu la kuzindua na kuhamasisha jamii kuhusu masuala ambayo yanatishia kuzisambaratisha. Kazi hizi ni kielelezo cha yale yanayopatikana katika jamii ya mwandishi. Katika jamii nyingi zetu siku hizi, kuna madai kuwa mtoto wa kiume ameachiliwa na yamkini hakuna sera nyingi za kiserikali zinazomshughulikia mtoto huyu ikilinganishwa na sera nyingi zilizoko za kumshughulikia mtoto wa kike hasa katika elimu. Masuala haya yanajitokeza katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau.*

## 3.5 MITAZAMO YA WATOTO WA KIKE KUHUSU WENZAO WA KIUME

Katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* inadhihirika kwamba uhusiano baina ya watoto wa kike na wa kiume ni uhusiano wa kufaana kidugu. Kila mmoja anamheshimu mwenzake. Hakuna anayemdharau au kumpuuza mwenzake. Wanatakiana mema na wanapenda kupata maendeleo pamoja. Maria alipenda kumsaidia ndugu yake. Kwa mfano Maria anamwamsha Juma aliyelala fofofo waende shuleni huku akimkumbusha kuwa mtihani ulikaribia. Mwishoni mwa hadithi Maria anapojitokeza kama mshauri kwa Juma, Juma anaanza kuiga kila kizuri alichofanya Maria. Juma anaelekea kutamani kuishi kama Maria.

Uhusiano mwema ulioko kati ya Juma na Maria ni dhihirisho la umoja ulioko miongoni mwa watoto katika jamii. Ushirikiana ni jambo muhimu kwa watu wowote

wale kwa ajili ya mafanikio na ni dhahiri kutokana na hadithi hii kuwa watoto hufanikiwa katika utangamano wao kwenye jamii kutokana na umoja walio nao licha ya tofauti zao zozote ambazo zaweza kuwepo.

## 3.6 HITIMISHO

Katika sura hii tumejadili usawiri wa watoto katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau.* Tumeanza kwa kutoa muhtasari wa hadithi yenyewe ambapo tumeona kuwa hadithi inahusu watoto wawili, Juma na Maria, ambao ni mapacha lakini tabia zao ni tofauti kabisa. Maria ana juhudi na huzingatia anayotakiwa kufanya, Juma ni mzembe na mwepesi wa kusahau. Tabia hizi zinamfanya Juma aaibike siku moja shuleni wakati wa paredi. Maria kwa upande wake anatuzwa kwa kuwa mwanafunzi safi zaidi. Tumeangazia taswira zinazobainika za mtoto wa kike na zile za mtoto wa kiume na kuona kuwa msichana amesawiriwa kwa njia chanya kama mhusika mwema na mwaadilifu huku mvulana akisawiriwa kwa njia hasi kama mtoto mwenye tabia mbaya. Tumetamatisha sehemu hii kwa kujadili mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume na ikabainika kuwa licha ya kusawiriwa kwa njia zilizotofautiana, watoto wana umoja wa hali ya juu na uhusiano baina ya watoto wa kike na wale wa kiume ni uhusiano wa karibu sana. Kila mmoja anamheshimu mwenzake. Hakuna anayemdunisha mwenzake.

Kutokana na utafiti wetu tumeona kuwa hadithi hii ya watoto ni kielelezo cha yale yanayopatikana katika jamii ya mwandishi. Katika jamii zetu siku hizi, kuna maoni kuwa mtoto wa kiume amesahauliwa huku asasi za kijamii kama vile familia na shule zikiendelea kumjali mtoto wa kike kuliko wa kiume.

# SURA YA NNE

# USAWIRI WA WATOTO KATIKA *LIKIZO YA MKOSI*

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tumejadili usawiri wa watoto katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi*. Tumeanza kwa kutoa muhtasari wa hadithi yenyewe kisha tukaangazia taswira zinazobainika za mtoto wa kike na zile za mtoto wa kiume. Vilevile, tumelinganisha usawiri wa watoto wa kike na wale wa kiume ili kuona kama kuna wale wanaosawiriwa kwa njia chanya kuliko wengine. Kadhalika, tumejadili mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume kwa kutathmini uhusiano wao. Hatimaye, tumejadili taswira za jumla za watoto wa kike na wa kiume katika jamii.

## 4.1 MUHTASARI WA *LIKIZO YA MKOSI*

*Likizo ya Mkosi* ni hadithi inayowalenga watoto hasa wa darasa la sita katika shule za msingi. Katika hadithi hii wahusika wakuu ni msichana Kerubo na ndugu yake Otambo. Tunakutana nao katika hekaheka zao za likizo.

Shule zilipofungwa kwa likizo ya muhula wa tatu Otambo na dada yake Kerubo, walitaka sana kwenda sehemu za mashambani kuwasalimia babu na nyanya yao huko Kisii. Baba yao, ambaye alikuwa mtafiti katika kampuni ya majani chai alikuwa amewaahidi kuwa angewapeleka mashambani iwapo wangeibuka wa kwanza katika mitihani ya mwisho wa muhula. Kerubo na Otambo walikuwa wanafunzi katika shule ya msingi ya Majimazuri Otambo katika darasa la tano na dada yake katika darasa la sita. Muhula huo walikuwa wametimiza ndoto zao na ya baba yao kwa kuibuka wanafunzi bora katika madarasa yao.

Baada ya shule kufungwa walienda nyumbani wakijua kuwa baba yao hangekuwa na kisingizio cha kukataa kuwapeleka mashambani wakawaone babu na nyanya yao. Walipofika nyumbani walimwonyesha mama yao matokeo yao mazuri. Baba yao alifurahishwa na matokeo yale mazuri na akakubali kutimiza ahadi yake ya kuwapeleka mashambani kuwajulia hali nyanya na babu yao. Aliwambia wajiandae awapeleke siku ya Jumapili wakae huko likizo nzima. Otambo na Kerubo walipakia nguo kwenye sanduku tayari kwa safari. Walibeba pia vitabu vya kusoma. Walikuwa tayari kwa safari. Kabla ya safari waliamua kubeba zawadi za kuwapelekea nyanya na babu. Walienda kwa Mzee Jumbe wakaomba majani ya Mchikichi ili kutemngenezea nyanya zawadi ya ufagio. Walipomaliza kuutengeneza ufagio waliupakia kwenye karatasi.

Siku ya safari Otambo na Kerubo waliamka mapema na kujiandaa. Walivaa nguo zao nzuri za safari. Walisaidiana kubeba sanduku lao lenye nguo hadi sebuleni. Walichukua mikoba yao ya vitabu. Mama yao tayari alikuwa amewaandalia kiamsha kinywa. Baada ya mashauri kutoka kwa wazazi wao waliingia garini na baba yao akashika usukani kuwapeleka kisha yeye arudi ili aende safari yake ya kikazi huko Tanzania. Mama alibaki nyumbani kutunza nyumba. Njiani walinunua fimbo ya kumpelekea babu yao. Walipofika mjini Kisii walinunua bidhaa za dukani kuwapelekea babu na nyanya. Walifika nyumbani kwa babu na nyanya mwendo wa saa sita adhuhuri.

Wajukuu walikaribishwa nyumbani kwao kwa hoi hoi na taadhima kuu. Walichinjiwa kuku. Baada ya kula, baba yao aliondoka ili aende akajiandae kwa safari ya Tanzania. Kerubo na Otambo waliwakabidhi babu na nyanya zawadi zao. Walizifurahia sana huku kila mmoja akitoa sababu kuonyesha kuwa zile zawadi ziliwafaa sana. Nyanya

alishukuru akisema ufagio wake ulikuwa tayari umechakaa na hivyo zawadi ya ufagio ilikuwa muhimu sana. Babu naye alisema bakora aliyokuwa akitumia ilikuwa imevunjika na hivyo hiyo mpya ingemfaa sana.

Walipomaliza kula chakula cha jioni, Kerubo alimsihi nyanya awasimulie hadithi. Nyanya alikubali. Aliwasimulia hadithi kuhusu vile punda alivyohusika katika kusababisha madoadoa katika ngozi ya wanyama wenzake kama vile chui, duma na fisi. Otambo na Kerubo waliajabia ile hadithi na hata walifungua kile kitabu cha picha za wanyama kuona jinsi walivyokuwa na madoadoa. Usiku huo walilala huku wakiwa na furaha nyingi.

Likizo ya Otambo na Kerubo katika sehemu za mashambani ilikuwa yenye shughuli nyingi za kila siku. Kerubo na Otambo waliwasaidia nyanya na babu kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kuwalisha kuku, kuwapa maji ya kunywa na kukusanya mayai na kisha kuyapanga mayai kwenye trei ili kwenda kuyauza sokoni. Baada ya shughuli kama hizo waliomba ruhusa kwenda kucheza na watoto marafiki wao wapya katika boma jirani. Waliweza pia kuwa na mijadala mbalimbali na watoto hao wenzao. Aidha, walisoma vitabu vyao kwa ajili ya kufanya marudio ili kuboresha masomo waliyofanya vibaya muhula uliokuwa umepita.

Siku moja waliandamana na nyanya kwenda Tabaka kuuza mayai. Babu alimtuma nyanya amnunulie gazeti. Walipomaliza kuuza mayai walipitia kwa muuzaji wa magezeti na kumnunulia babu gazeti la *Mwananchi*. Walipokuwa wanatembea kurudi nyumbani, Otambo alianza kupitia gazeti hilo harakaharaka. Alipofungua kurasa za katikati za gazeti hilo, alipigwa na butwaa kuona picha ya baba yake akiwa amelazwa hospitalini. Aliwaonyesha nyanya na Kerubo huku akiwa ameshtuka. Walisoma na

kuona kuwa baba yao alikuwa amehusika katika ajali ya barabara akitoka Arusha, Tanzania kwenda Nairobi. Wote walijawa na hofu.

Walipofika nyumbani na kumuonyesha babu habari zile gazetini, nyanya alishauri ilikuwa bora wafunge safari mara moja hadi Nairobi kumjulia hali mwanao.

Walipofika katika hospitali ya Nairobi, Kerubo na Otambo walifurahi kumwona baba yao akiwa salama. Babu na nyanya pia walifurahi. Kerubo alisema kwamba hiyo ilikuwa likizo ya mkosi lakini walishukuru Mungu kwa kumlinda na kumnusuru baba yao. Wote walikubaliana na usemi wa Kerubo.

## 4.2 TASWIRA ZINAZOBAINIKA ZA MTOTO WA KIKE

Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* mtoto wa kike anawakilishwa na mhusika Kerubo ilhali wa kiume anawakilishwa na mhusika Otambo. Taswira kuu tunayopata ya msichana ni kuwa amempiku mvulana kwa mambo mengi.

Mtoto wa kike kusawiriwa kama aliyempiku mtoto wa kiume ni jambo ambalo limejitokeza tangu mwanzoni na kuendelea hadi mwishoni mwa kisa. Shuleni kwa mfano, Kerubo aonekana kupendelewa kwa kutuzwa zawadi ya thamani zaidi kuliko Otambo ingawa wote wawili walikuwa wamefanya vizuri masomoni. Kerubo anapewa kitabu cha hadithi ya *Hazina ya Zuena na Makombo* ili ajifunze mbinu muhimu maishani ya kuweka akiba. Otambo kwa upande wake, alituzwa zawadi ya kitabu cha picha za wanyama pori na ndege. Ingawa vitabu vyote viwili vina mafunzo muhimu, inaweza kudaiwa kuwa mafunzo ya kitabu cha Kerubo yangekuwa na umuhimu mkubwa zaidi kwa kuwa uwekaji wa hazina ni mbinu muhimu katika maisha ya kila mtu kote ulimwenguni. Mwalimu wa Kerubo alitaka ajifunze uwekaji wa hazina ilhali mwalimu wa Otambo haelekei kuwa na lolote la Otambo kujifunza

ila kujiburudisha kwa picha za wanyama na ndege. Katika maisha ya kawaida wanyama na ndege hasa wa pori huwa ni kivutio kama vile cha watalii ambapo lengo kuu la kuwatazama huwa ni kujiburudisha. Nyumbani, kitabu cha Kerubo kilisifiwa na mama yao kabla ya kile cha Otambo. Hata ikambidi Otambo kumuuliza mama yake:

*"Na changu mama...?"* (Uk 6)

Tukio hili laelekea kuonyesha kuwa baadhi ya wanajamii wakiwemo walimu shuleni na hata baadhi ya wazazi nyumbani hufikiria watoto wa kike kuliko wale wa kiume. Watoto wa kike wasawiriwa kama wanaowapenda baba zao sana. Kwa mfano, mwishoni mwa hadithi, Kerubo alionekana kuwa na wasiwasi mwingi kuliko Otambo baada ya kuona picha ya baba yao akiwa hospitalini. Hata inambidi babu yao amtulize kwa kumwambia asitie tumbo moto kwani baba yao alikuwa salama salimini.

Jambo hili linaambatana na dhana katika jamii nyingi kuwa watoto wa kike huwapenda baba zao kuliko pengine wanavyowapenda mama zao.

Kimawazo, msichana anasawiriwa kama aliyekuwa mwepesi wa kufikiri. Mara nyingi Kerubo anaonekana kuwaza haraka kuliko Otambo na kutoa kauli yake. Kwa mfano, walipokuwa wakielekea nyumbani baada ya ushindi wao shuleni, Kerubo ndiye aliyekuwa wa kwanza kutoa maoni kuwa baba yao hangekuwa na kizingizio cha kukataa kuwapeleka kwenda kuwasalimia babu na nyanya yao. Pia, Kerubo ndiye aliyetangulia kumwambia mama yao walipofika nyumbani baada ya kufunga shule kwamba walikuwa wamefanya vizuri muhula huo. Aidha, Kerubo ndiye aliyetangulia kumwambia mama yao kuwa walikusudia kuwapelekea nyanya na babu zawadi. Ndiye pia aliyeamua aina ya zawadi ambayo wangenunua kama ifuatavyo:

> "Umefikiria kuhusu zawadi tutakazowapelekea nyanya na babu?" Otambo akamuuliza Kerubo.

> Kerubo alinyamaza kwa muda mrefu kisha akajibu, "Nafikiri nyanya atapenda sana ufagio. Tunaweza kumtengenezea ufagio kwa kutumia matawi ya Mchikichi."
> "Na babu je?" Otambo akauliza.
> "Tutamnunulia fimbo umbo la nambari '7' atakayotumia kutembea," Kerubo akajibu.
> Otambo alikubaliana na dada yake kuhusu suala la zawadi ambazo wangewapelekea nyanya na babu yao. (Uk 13)

Kerubo alipendekeza nyanya yao apelekewe ufagio na babu apewe fimbo.

Msichana amechorwa pia kama mwenye kukumbuka mambo haraka. Kwa mfano. Kerubo, Otambo na baba yao walipokuwa njiani wakielekea kwa nyanya, Kerubo ndiye aliyetanabahi kuwa walisahau kumnunulia babu zawadi yake ya fimbo. Baadaye wakiwa kwa nyanya, yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kukumbuka kumwomba nyanya awasimulie hadithi baada ya chakula cha jioni.

Msichana amesawiriwa akiwa mwepesi wa kutenda kuliko mvulana. Kwa mfano walipofika nyumbani kutoka shuleni, Kerubo alimtangulia Otambo kuingia chumbani mwake na kuvua sare yake ya shule na kuvaa nguo za nyumbani. Kerubo pia alipangusa meza haraka baada ya kula. Kerubo hali kadhalika aliweza kujipatia marafiki wawili ilhali Otambo alikuwa na rafiki mmoja tu kule kwa nyanya yao.

Mtoto wa kike ni mwenye akili tambuzi. Kerubo aligundua kuwa kitabu cha Otambo kilikuwa na sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ilikuwa na picha za wanyamapori na sehemu ya pili picha za ndege. Alikuwa pia wa kwanza kusikia mama yao akiwaitia chakula.

Msichana amesawiriwa kama mshauri wa mvulana. Kerubo anamshauri Otambo asizungumze akiwa na chakula mdomoni kwa kusema:

> "Meza chakula kwanza. Hukumbuki alivyotuambia mwalimu Kazungu kuwa ni tabia mbaya kuzungumza huku ukitafuna chakula!" Kerubo alimshauri Otambo. (Uk 8)

Kerubo alimkumbusha Otambo kuwa mwalimu wao aliwaambia ni tabia mbaya mtu kuzungumza huku akitafuna chakula.

Msichana anaonekana akiwa mwenye kupenda amani. Kerubo na Rodah, ambaye alikuwa msichana mwenzake, wanakomesha ugomvi dhidi ya Otambo na Mageka na kuweza kuwashawishi waache kugombana. Msichana ni mshauri mwenye ujuzi hata wa kushauri akitumia methali za Kiswahili. Kwa mfano, Kerubo anawashauri Otambo na Mageka kwa methali kuwa asiyekubali kushindwa si mshindani na hivyo waache upuzi wasipigane:

> "Acheni mara moja. Huu ni upuuzi mtupu. Asiyekubali kushindwa si mshindani," Kerubo na Rodah waliingilia kati kukomesha ndugu zao wasipigane.
> "Kumbuka mama alituambia tuwe na nidhamu," Kerubo alimkumbusha Otambo ambaye alikuwa na hasira kama mkizi. (Uk 34)

Mwandishi anawafunza watoto kuwa hawafai kuwa na chuki. Watoto wanaosoma hadithi hii wanaweza kuamini mambo kama haya kwa kuwa katika jamii wavulana wakati mwingine hugombana na pengine wasichana wakajaribu kuwasihi waache ugomvi.

Usawiri mwingine tunaopata katika utafiti wetu ni kuwa Kerubo ni msichana mbunifu. Mathalani, mwishoni mwa kisa hiki ndiye aliyeibuka na kauli kuwa hiyo ilikuwa likizo ya mkosi. Hadithi hii ya watoto imepewa anwani *Likizo ya Mkosi* kutokana na usemi huu wa Kerubo.

## 4.3 TASWIRA ZINAZODHIHIRIKA ZA MTOTO WA KIUME

Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* mvulana amesawiriwa kama anayetanguliwa na msichana katika mambo mengi na hata wakati anapotangulia kutoa maoni yake, anatoa kauli ambazo wakati mwingine zimeambatana na kasoro zinazostahili kurekebishwa. Mfano mmoja ni wakati Otambo anatangulia kuuliza juu ya safari yao ya mashambani lakini inatokea kwamba anatadhaharishwa na Kerubo kuwa amefanya kosa la kuzungumza kabla ya kumeza chakula. Kerubo anamwambia:

> "Meza chakula kwanza hukumbuki alivyotuambia mwalimu Kazungu kuwa ni tabia mbaya kuzungumza huku ukitafuna chakula!" Otambo alimeza chaukula kwanza na kusuma "Samahani." (Uk 8)

Hata hivyo, mvulana anasawiriwa kama mwenye adabu wakati Otambo anapokubali kuomba msamaha anaposhauriwa na Kerubo kumeza chakula kwanza badala ya kuongea akiwa na chakula kinywani.

Mfano mwingine wa msichana kumpiku mvulana ni wakati ambapo Otambo alipendekeza wawapelekee babu na nyanya zawadi lakini akashindwa kuamua haraka ni zawadi gani iliyofaa na hatimaye akamtegemea Kerubo katika kuamua ni zawadi gani iliyofaa. Baada ya kuchukua muda wa kufikiria kuhusu zawadi, Otambo anamuuliza Kerubo:

> "Umefikiria kuhusu zawadi tutakayowapelekea nyanya na babu?" (Uk 13)

Mvulana amesawiriwa kama mwenye hasira za haraka. Kwa mfano, wakati wa mjadala kuhusu maisha ya mjini yakilinganishwa na maisha ya mashambani, Otambo

anachukiana na mvulana mwenzake aliyeitwa Mageka baada ya mjadala kupamba moto. Wanashikana mashati na kutaka kurushiana makonde.

Jambo lingine muhimu linalobainika katika hadithi hii ya *Likizo ya Mkosi* ni kuwa malezi ya watoto huwa bora panapokuwepa na ushirikiano wa wazazi wote wawili, yaani baba na mama. Kerubo na Otambo wanaonekana wakishauriana na wazazi wao wawili mara kwa mara na tunaweza kuchukulia kuwa ni kwa sababu hii tabia ya Otambo ikawa si mbaya kama ilivyo ya Juma katika *Mwepesi wa Kusahau.* Baba yake Juma hakuonekana katika maisha ya kila siku ya Juma na Maria. Alitajwa tu na haonekani akishawishi jambo lolote baadaye kama anavyoonekana baba yake Otambo ambaye yuko na watoto wake katika kila hatua ya maisha yao hadi pale anaposafiri kwenda Tanzania kikazi.

Jambo hili ni kielelezo cha maisha ya kawaida katika jamii ambapo katika asasi ya familia, watoto wa kiume hukabiliwa na changamoto nyingi ikiwa baba yao hayuko au hana wakati wa kutekeleza majumu yake kwa watoto hasa kuwa nao na kuwashauri kuhusu masomo na maisha kwa jumla. Baba yake Juma hahusiki katika maisha ya Juma na Maria kama ambavyo baba yake Otambo anavyohusika katika maisha ya watoto wake.

Katika jamii zetu aghalabu huwa kuna changamoto nyingi zaidi zinazowakabili watoto wa kiume wapokua bila baba yao kushiriki katika maisha yao ya kila siku.

## 4.4 ULINGANISHI WA USAWIRI WA WATOTO WA KIKE NA WA KIUME KATIKA *LIKIZO YA MKOSI*

Ingawa tofauti ya usawiri wa msichana na mvulana si pana sana katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* kama ilivyo katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau,* kinachojitokeza wazi ni kuwa msichana yuko hatua mbele ya mvulana katika kila jambo.

Mathalani, msichana ni mwepesi zaidi kufiri na kutoa mawazo yake kuliko mvulana. Kerubo mara kwa mara anamkata kauli Otambo pengine kwa kutaka kutoa maelezo mwafaka zaidi. Kwa mfano wakati walipoenda kumuomba Mzee Jumbe matawi ya Mchikichi Mzee Jumbe anapouliza matawi ni ya nini Otambo ananza kwa kutoa maelezo yasiyoonekana kuwa ya moja kwa moja na ndipo Kerubo anapomkata kauli na kutoa maelezo yanayolenga jibu moja kwa moja kwa kusema matawi ni ya kutemngenezea nyanya zawadi ya ufagio.

> "Tunataka kutumia matawi hayo kumtengenezea nyanya yetu zawadi ya ufagio," Kerubo akamkata usemi Otambo. (Uk 15)

## 4.5 MITAZAMO YA WATOTO WA KIKE KUHUSU WENZAO WA KIUME

Utafiti wetu ulithibitisha kuwa watoto wa kike na wale wa kiume wana umoja na ushirikiano mkubwa. Wao hupenda kufanya mambo mengi yao pamoja. Wanashirikiana kufanya kazi. Kwa mfano, Kerubo na Otambo waliondoa vyombo mezani pamoja walipomaliza kunywa chai wakiwa kwao nyumbani. Pia, Kerubo alipokuwa anapangusa meza naye Otambo alishiriki kwa kufagia sakafu na kupanga viti. Walishirikiana pia kutafuta majani ya Mchikichi ili kumtengenezea nyanya ufagio kisha walitengeneza ufagio pamoja. Katika ukurasa wa 13 tunaambiwa hivi:

> Kerubo na Otambo walimaliza kunywa chai. Wakaondoa vyombo mezani. Kerubo alipokuwa anapangusa meza, Otambo alifagia sakafu na kupanga viti. Hatimaye wote walitoka nyumbani kwenda kutafuta matawi ya Mchikichi ili kumtengenezea nyanya yao zawadi ya ufagio. (Uk 13)

Baadaye wanashirikiana kwenda hadi ilikokuwa mizigo yao kuwaletea babu na nyanya zawadi zao. Otambo anabeba fimbo naye Kerubo anabeba ufagio.

Ushirikiano huu unathibitisha kuwa watoto wa kike na wa kiume hawabaguani. Hakuna majukumu wanayotengewa wale wa kiume ama wale wa kike pekee. Watoto wa kiume na wa kike wanashauriana na kuheshimiana. Kerubo anamshauri Otambo asizungumze akiwa na chakula kinywani na Otambo anatii. Otambo pia anamshauri Kerubo asisahau kubeba vitabu vya kusoma. Kerubo pia alitii na kusema kuwa angebeba vitabu vya masomo ambayo hakuwa amepata alama za kuridhisha.

Watoto hawayadharau mawazo ya wenzao wala kuyadunisha. Wanachangiana kimawazo. Kwa mfano, Otambo anaposema kuwa ana hamu ya kuwaona nyanya na babu kwa kuwa wana ushauri mzuri, Kerubo anachangia wazo hili na kulikuza zaidi kwa kumkata kauli Otambo na kuongeza kuwa mbali na ushauri nyanya atawasimulia hadithi za kupendeza na za kuelimisha sana.

Vilevile Otambo anapopendekeza wawapelekee nyanya na babu zawadi, Kerubo anakubali kuwa ni wazo zuri sana na anachangia zaidi kwa kuuliza ni zawadi gani wangewapelekea. Otambo naye anamuuliza Kerubo ikiwa alikuwa na maoni yoyote kuhusu aina ya zawadi iliyofaa. Mwishowe wanakubaliana wachukue muda kufikiria. Hatimaye Otambo alikubaliana na dadake kuhusu suala la zawadi ambazo wangewapelekea nyanya na babu yao. Aidha, wanapoongea pamoja hadi inakuwa usiku, Kerubo anapendekeza walale na ingawa Otambo hakutaka kulala mwanzoni, alibadilisha nia na kukubaliana na Kerubo kuwa walale.

Kutokana na matukio haya tunaona kuwa watoto wanasawiriwa kama watu wanaoheshimu maoni ya kila mtoto mwenzao bila kujali kama maoni yalitolewa na wa kike au wa kiume.

Matukio haya ni kielelezo cha maisha ya kawaida ya watoto katika mazingira ya shule na nyumbani.

## 4.6 TASWIRA ZA JUMLA ZA WATOTO WA KIKE NA WA KIUME

Hadithi ya *Likizo ya Mkosi* imefaulu kutupatia taswira za jumla za watoto katika jamii zetu wawe wa kike au wa kiume.

Watoto wanasawiriwa kama wajasiri na wanaopenda kujaribu mambo mageni ili kufanya ugunduzi. Kwa mfano wakati wa safari ya mashambani, Otambo anasema wao wanaweza kujipeleka kutoka jijini walikoishi hadi Kisii peke yao naye Kerubo anawalaumu kwa ujasiri wazazi wao kuwa wao ndio wamewafanya wasijue lugha ya kwao nyumbani ya Ekegusii kwa kukosa kuwapeleka nyumbani.

Watoto wamesawiriwa pia kama waaminifu na watiifu. Kwa mfano, wote wawili wanaahidi kuwa hawatawasumbua nyanya na babu na watakuwa na nidhamu ya hali ya juu wakifika kwa nyanya. Walifanya kama walivyoahidi wakati walipokaa kwa nyaya yao. Wote wawili walitii wito wa baba yao na kuwa wenye nidhamu walipokuwa kwa babu na nyanya.

Watoto wamechorwa kama wanaopenda kujitolea kusaidia kwa hiari. Kwa mfano, Kerubo na Otambo wanajitolea kumsaidia baba yao kubeba bidhaa walizonunua dukani hadi ilipoegeshwa gari. Kadhalika walimsaidia nyanya yao kuwasha jiko na kulipepeta kwa zamu. Waliwasaidia babu na nyanya katika shughuli za shambani

kama vile kupakia matunda. Kerubo pia alimsaidia nyanya yake kufanya kazi za nyumbani.

Watoto wa kiume na wa kike wanaonekana wakiwa wenye roho safi. Kwa mfano, Kerubo na Otambo wanawapungia mkono watoto hata wasiowajua kule kijijini ili kuwajibu watoto waliokuwa wakilipungia gari lao mkono lilipofika katika barabara za mashambani.

Kadhalika watoto wamesawiriwa kama wadadisi. Mathalani, Kerubo alitaka kujua ugonjwa wa majani chai wa *Armillaria Mellae* ni gani aliposikia baba yake ameutaja kwa mara ya kwanza na pia alitaka kujua vile vinyago walivyoona vikitengenezwa viliuzwa wapi. Kwa upande wake, Otambo naye anauliza nchi za Maziwa Makuu ni zipi baada ya kusikia baba yao akizitaja.

Watoto huwa na adabu na heshima kwa wakubwa. Katika hadithi tuliyosoma tuliona Kerubo na Otambo wanapomwomba Mzee Jumbe matawi ya Mchikichi wanamzungumzia kwa kutumia msamiati wa adabu na heshima. Walimsabahi kwa pamoja kwa kumwambia:

> "Shikamoo Mzee Jumbe?" Kisha Otambo akasema "Tafadhali tunakuomba ruhusa ya kuchuma matawi ya Mchikichi."
> Waliporuhusiwa wote wawili walikumbuka kushukuru kwa kusema "Asante sana." (Uk 14)

Watoto wanasawiriwa kama wanaowapenda nyanya na babu. Walitamani sana kuwatembelea kwao mashambani. Aidha, walishughulika kuwatafutia zawadi ambazo

zingewapendeza. Jambo hili linaakisi hali katika jamii zetu ambapo watoto wadogo hufurahia sana kupelekwa kwenda kuwaona nyanya na babu.

Watoto wanasawiriwa kama walio wabunifu. Kerubo na Otambo waliwaza juu ya aina za zawadi bora za kuwapelekea babu na nyanya hadi wakaibuka na zawadi inayomfaa kila mmoja kulingana na mahitaji yake – babu fimbo yenye umbo la nambari '7' na nyanya ufagio. Walijua kuwa fimbo ingekuwa mkongojo wa kumsaidia babu kutembea ilhali ufagio ungemsaidia nyanya kufagia. Ilisadifu baadaye kuwa ufagio ungemfaa nyanya sana kwa vile wake ulikuwa umechakaa huku fimbo nayo ikimfaa babu sana kwa kuwa yake ilikuwa imevunjika akimpiga fahali wake mtundu.

Katika utafiti wetu tuliona kuwa sifa hizi zinaweza kulingana na za watoto katika jamii zetu za Kiafrika. Katika jamii zetu watoto kwa kawaida huridhika kwa dhati juhudi zao zinapozaa matunda. Haya yanaonekana kupitia kwa Kerubo na Otambo wakati matokeo yao mazuri ya mtihani yaliwafurahisha sana. Pia waliridhika walipofaulu kutengeneza ufagio.

Kwa mujibu wa nadharia ya sosholojia ya fasihi, mambo haya wamewasilishwa kwa njia ambayo msomaji anaweza kuyaona kama kielelezo cha hali ilivyo katika jamii kwa sababu matendo yanayofanywa na watoto wahusika yanalingana na matendo mbalimbali yanayofanywa na watoto katika jamii. Ni kawaida kuwaona watoto wakiwa na hulka kama hizi za Kerubo na Otambo katika jamii zetu. Kwa mfano, watoto hufanya bidii masomoni wanapoahidiwa zawadi kama vile ile safari waliyoahidiwa akina Kerubo ya kwenda kwa nyanya. Wao hupenda kuwakumbusha

wazazi juu ya ahadi walizotoa kama Kerubo na Otambo walivyowakumbusha wazazi wao juu ya ahadi waliyowapa ya kwenda kwa nyanya iwapo wangefanya vizuri masomoni.

Watoto wengi katika jamii zetu hasa wale wadogo wawe wa kike au wa kiume wana tabia nyingi zinazofanana na za kina Kerubo kama vile kuwa ni wajasiri, wanaopenda kujaribu mambo mageni ili kugundua, ni wadadisi, waaminifu, hupenda kusaidia wazazi kazi na ni wenye roho safi. Kutokana na tathmini yetu inayoongozwa na sosholojia ya fasihi tunaona tabia hizi za Kerubo na Otambo kama watoto, ni kielelezo cha tabia za watoto halisi katika jamii ya kawaida.

## 4.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumejadili usawiri wa watoto katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi*. Tumeanza kwa kutoa muhtasari wa hadithi yenyewe ambapo tumeona kuwa hadithi inahusu wahusika wakuu wawili ambao ni watoto wajulikanao kama Kerubo na ndugu yake Otambo. Tumeona kuwa ingawa tofauti ya usawiri wa msichana na mvulana si pana sana katika hadithi hii ya *Likizo ya Mkosi* kama ilivyo katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* bado inadhihirika kwamba msichana anampiku mvulana katika mambo mengi. Tumeangazia taswira zinazobainika za mtoto wa kike na zile za mtoto wa kiume na kuona kuwa msichana amesawiriwa kwa njia chanya kama mhusika ambaye aghalabu anamtangulia mvulana kufikiri na kufanya maamuzi. Tumetamatisha sehemu hii kwa kujadili mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume na ikabainika kuwa uhusiano baina ya watoto wa kike na wale wa kiume ni uhusiano wa karibu sana. Kila mmoja anamheshimu mwenzake na hakuna anayemdunisha mwenzake. Wote wanapenda kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano.

Katika hadithi hii, imebainika pia kuwa malezi ya watoto huwa bora panapokuwepa na ushirikiano wa wazazi wote wawili. Kerubo na Otambo wanaonekana wakishauriana na wazazi wao wawili yaani baba na mama mara kwa mara na hivyo basi tabia ya Otambo si mbaya kama ilivyo ya Juma. Baba yake Juma haonekani katika maisha ya kila siku ya Juma na Maria. Alitajwa tu pale mwanzoni na haonekani akiwaelekeza katika maisha yao ya kila siku kama anavyoonekana baba yake Otambo ambaye yuko na watoto wake katika kila hatua ya maisha yao.

Jambo hili ni kielelezo cha maisha ya kawaida katika jamii ambapo katika asasi ya familia, watoto wa kiume hukabiliwa na changamoto nyingi ikiwa baba yao hayuko au hana wakati wa kutekeleza majumu yake kwa watoto hasa kuwa nao na kuwashauri kuhusu masomo na maisha kwa jumla.

Usawiri huu wa mwandishi ni kioo au kielelezo cha sifa na vituko vya watoto katika jamii. Kwa kuangalia matukio haya katika mtazamo wa nadharia ya sosholojia ya fasihi, tuliona kuwa watoto wengi wa rika la Kerubo na Otambo huwa na sifa kama za wahusika hao. Kuwepo kwa mambo ambayo ni kielelezo cha yale yanayojiri katika jamii kunaimarisha upokezi wa hadithi miongoni mwa watoto kwa kuwa watoto hujiona kupitia kwa ile hadithi. Ukweli huu unachangia matukio kuwa kielelezo cha maisha ya baadhi ya watoto nyumbani na shuleni katika jamii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kubainisha usawiri wa watoto katika hadithi za watoto za Kiswahili. Ili kuafikia lengo letu tulichunguza hadithi mbili ambazo ni *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*. Kutokana na utafiti huu, hadithi hizi zimeonekana kuinua hadhi ya mtoto wa kike juu ya yule wa kiume.

## 5.1 MUHTASARI

Katika utafiti huu, mada yetu imehusu usawiri wa watoto katika vitabu vya hadithi za watoto. Vitabu tulivyohakiki vilikuwa *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*. Kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti huu, ambayo yalikuwa kubainisha taswira za mtoto wa kike zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi;* kubainisha taswira za mtoto wa kiume zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi;* kulinganisha sifa za watoto wa kike na wenzao wa kiume na kuchunguza mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume katika *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*; tulijadili taswira zinazobainika za mtoto wa kike na za mtoto wa kiume katika hadithi hizo mbili. Aidha, tulilinganisha usawiri wa watoto wa kike na wale wa kiume katika hadithi hizo na kisha kutathimini mitazamo ya watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume kama inavyojitokeza katika hadithi husika.

Nadhariatete mbili zilizoongoza utafiti huu ni kwamba katika hadithi za watoto, msichana huchorwa akiwa mwema kuliko mvulana na pili ni kuwa wasichana na wavulana katika jamii ya sasa wanajiona kuwa sawa. Kupitia kwa utafiti huu nadhariatete zote mbili zilithibitishwa kuwa kweli.

Nadhariatete ya kwanza inadhihirika dhahiri hasa kupitia matukio katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* ambapo mtoto wa kike anasawiriwa kwa njia chanya zaidi kuliko mtoto wa kiume. Mtoto wa kike, Maria, anasawiriwa kama mwenye kuwajibika katika shughuli zake zote nyumbani na shuleni ilhali Juma, ambaye ni mtoto wa kiume, anasawiriwa kama mtu asiyejali akiwa nyumbani na hata shuleni.

Nadhariatete ya pili inathibitika waziwazi hasa kupitia katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* ambapo uchunguzi wa mahusiano ya mtoto wa kike, anayewakilishwa na mhusika Kerubo na wa kiume anayewakilishwa na Otambo, unaonyesha kuwa watoto wa kike na wale wa kiume wana umoja na ushirikiano mkubwa. Wao hupenda kufanya mambo mengi yao pamoja. Wanashirikiana kufanya kazi na hawabaguani. Hakuna majukumu wanayotengewa wale wa kiume ama wale wa kike.

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya sosholojia ya fasihi kwa vile tuliona kuwa nadharia hii ingetusaidia katika uchambuzi wetu wa jinsi watoto wanavyosawiriwa kwa kuwa ina uwezo mkubwa wa kuchanganua maswala yanayohusu jamii hasa ikikumbukwa kuwa fasihi ni zao la jamii.

Usawiri wa watoto tuliopata katika hadithi tulizochunguza ni kielelezo cha yale yanayopatikana katika jamii ya mwandishi. Hii ni kwa kuwa mwandishi huathiriwa na mazingira yake pamoja na wanajamii anaotagusana nao. Maswala ya watoto wa kike katika jamii yamekuwa yakiangaziwa sana miaka ya hivi karibuni miongoni mwa wanajamii na katika vyombo vya habari. Haya yamepelekea wanajamii kuwa na

mwamko wa kutosha kuwatambua wasichana na kutambua haki zao kikamilifu na kuzitetea. Maudhui katika hadithi hizi yameashiria jinsi hali halisi ilivyo katika jamii zetu kwa kumulika jamii na jinsi mwonoulimwengu wayo ulivyo kuhusu mtoto wa kike.

## 5.2 MATOKEO YA UTAFITI

Kutokana na utafiti huu imethibitishwa kuwa hadithi mbili zilizochunguzwa katika utafiti huu zinamsawiri mtoto wa kike kwa njia chanya zaidi kuliko mtoto wa kiume. Hata hivyo, watoto wao wenyewe hawachukiani baina ya wale wa kike na wale wa kiume. Watoto wenyewe wamesawiriwa kama ambao wanapendana na wenye umoja.

Taswira za mtoto wa kike na wa kiume zinazojitokeza katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi* zilibainisha kuwa msichana amechorwa kwa mitazamo chanya katika hadithi zote mbili. Usawiri wa watoto wa kike na wa kiume unaojitokeza katika kazi tulizochunguza unatokana na hali iliyo katika jamii ya mwandishi. Kwa mtazamo wa nadharia ya sosholojia ya fasihi, hii ni ithibati kuwa jamii ya mwandishi ina mtazamo mzuri kuhusu mtoto wa kike. Jamii inamwona kama mwaadilifu, mwenye bidii, akili na mwelekeo. Msichana ni mfano bora wa kuigwa. Wasichana wamepewa nafasi muhimu katika hadithi hizi na yamkini hali hii ni kielelezo cha nafasi wanayopewa katika jamii ya mwandishi. Jambo hili limejitokeza wazi hasa katika *Mwepesi wa Kusahau* ambapo ilibainika wazi kuwa mtoto wa kike ameinuliwa kihadhi na yule wa kiume kubaki katika hali ya kuhuzunikiwa akiwa ameshindwa na msichana katika mambo mengi kama vile kudumisha usafi na maadili kwa jumla.

Kwa mfano, kupitia kwa mhusika Maria, katika *Mwepesi wa Kusahau*, tunakabiliana moja kwa moja na hali katika jamii ambapo mtoto wa kike anasawiriwa kwa njia chanya zaidi kuliko mtoto wa kiume. Mtoto wa kike, Maria, anasawiriwa akiwa mwenye kuwajibika katika shughuli zake zote nyumbani na shuleni ilhali Juma, ambaye ni mtoto wa kiume, anasawiriwa kama mtoto mchafu, asiyekumbuka mambo wala kujali. Maria amechorwa kama kielelezo cha jitihada za kibinafsi zinazomfanya mtu afaulu maishani.

Mikabala kama hii inaendelea kudumaza maendeleo ya mtoto wa kiume katika jamii zetu. Katika jamii na mandhari ambamo hadithi hizi zimeandikiwa masilahi ya mtoto wa kike yameendelea kutiliwa maanani huku ya mvulana yakipuuzwa. Hali hii ndiyo inayoakisiwa katika hadithi za watoto kama vile ile ya *Mwepesi wa Kusahau.* Anwani hii yenyewe inatokana na tabia hasi ya Juma ya kuwa mwepesi wa kusahau.

Kadhalika, dhana ya kuwainua wasichana na kuwapa nafasi sawa na wavulana inajitokeza katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi*. Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* msichana amesawiriwa akiwa hatua japo kidogo mbele ya mvulana katika matukio mbalimbali kwenye hadithi. Kwa mfano, Kerubo (ambaye ni msichana) amesawiriwa kama anayefanya maamuzi mengi yanayoelekeza mambo ambayo wanafanya pamoja na ndugu yake wa kiume Otambo.

Hata hivyo, kwa kutathimini mitazamo ya wahusika watoto wa kike kuhusu wenzao wa kiume katika hadithi za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi*, utafiti huu umeonyesha kuwa watoto wa kike na wale wa kiume wana uwezo mkubwa wa kushirikiana na kupenda kusaidiana licha ya tofauti zozote baina yao. Sifa hizi

zinaakisi uhalisia wa sifa za watoto maishani ambapo kwa mfano watoto waweza hupatikana wakishirikiana na kucheza pamoja bila kujali tofauti zozote zinazoweza kuweko baina yao. Sifa hizi zimetusaidia kudondoa mitazamo ya watoto wa kike kuhusu watoto wenzao wa kiume.

Kutokana na utafiti huu tumeona kuwa watoto wa kike na wale wa kiume wamesawiriwa kama wanaojiona sawa wao wenyewe. Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* ilibainika kuwa hakuna tena majukumu wazi ya watoto wa kiume wala yale ya wasichana pekee kama ilivyokuwa katika hadithi za hapo awali (nyingine ambazo zilirejelewa katika sura ya pili kama vile *Atendaye Mema* na *Bonde la Wafu*) ambapo wavulana walikuwa na majukumu kama vile kuwinda msituni huku wasichana wakibaki nyumbani.

Watoto wa kike na wa kiume wamechorwa kama wanaopendana, kuheshimiana na kushirikiana kutekeleza shughuli zao za kila siku.

## 5.3 HITIMISHO

Kwa muhtasari, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa watoto wa kike wametukuzwa na kusawiriwa kwa njia chanya kama wenye busara na bora kuliko wale wa kiume. Utafiti huu pia umeonyesha kuwa licha ya watoto wa kike kusawiriwa kama waliowapiku wenzao wa kiume masomoni na kwa mengine mengi maishani, watoto wenyewe hawachukiani na wanaendelea kusaidiana na kushirikiana maishani mwao.

Kwa kutathmini hali hii katika mtazamo wa nadharia ya sosholojia ya fasihi, hadithi za watoto za *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkosi* zinaonekana kuwa kielelezo

cha mitazamo ya jamii ya kipindi cha wakati tuliopo kuhusu watoto na mtazamo wa watoto wenyewe kuhusu watoto wenzao.

## 5.4 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Kutokana na matokeo ya utafiti huu inapendekezwa hatua za dharura zichukuliwe kumshughulikia mtoto wa kiume katika jamii ili kumwokoa kutoka hatari ya kubaki nyuma ya yule wa kike katika elimu na maendeleo mengine ya kijamii. Tulipokuwa tunashughulikia utafiti huu tuligundua kuwa katika baadhi ya jamii wototo wa kiume waliojiingiza katika utovu wa nidhamu wakiwa shuleni, kama vile Juma katika *Mwepesi wa Kusahau,* wameishia kuwa vijana walevi na wasiowajibika kwa lolote katika jamii zao.
Kwa vile fasihi haichipuki kutoka ombwe tupu bali ni kioo cha jamii, inatarajiwa kuwa jamii ikimjali mtoto wa kiume kama vile inavyomjali mtoto wa kike, usawiri wa mtoto wa kiume katika vitabu vya hadithi za watoto utaweza kuwa bora kuakisi hali yao itakayokuwa imeimarika katika jamii. Ni matumaini yetu kuwa wavulana watakaozisoma hadithi zenye mitazamo chanya kuwahusu watapata kichocheo cha kuwahamasisha kukua wakiwa watu wanaojiamini na wanaowajibika katika jamii.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu vipengele vingine vya ya fasihi ya watoto ya Kiswahili kama vile masuala ibuka katika fasihi ya watoto.

## MAREJELEO


Ahmed, A.H. (2003) *Kifimbo cha Cheza*. Nairobi: Oxford University Press.

Alembi, E. (2007) Phases and Dynamics in Children Literature in Kenya. In *The 10th Nairobi International Book Fair Booklet*. Nairobi: Kenya Publishers Association, 6-9.

Borg W.R. & Gall, M.D. (1993) *Educational Research: An Introduction*. New York: Longman Publishers Ltd.

Buliba, A. et al (2014) *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti.* Mwanza: Serengeti Education Publishers (T) Ltd.

Chacha, W.C. (2013) *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Nguzo Mama* na *Mama Ee.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Eagleton, T. (1996) *Literary Theory*. London: Blackwell Publishing.

Escarpit, R. (1966) *Sociology of Literature*. London: Frank and Cass.

Glicksberg, C.L. (1987) *Literature and Society: The Sociology of Literature.* (wh) Dandson P. Cambrige: Chadwik Harley.

Government Printers, (2010) *Katiba ya Kenya*. Nairobi.

Grenby, M.O. (2008) *Children's Literature*. Edinburg: Edinburg University Press.

Howe, F. (1970) Sexual Stereotypes Start Early in *The Study of Society* (mh) Peter I. Rose. New York: Random House 144 – 152.

Hunt, P. (mh) (1994) *An Introduction to Children Literature*. New York: Oxford University Press.

Kairu, W.M. (2005) *Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Karinge, J.W. (2013) *Usawiri wa Ndoa katika Riwaya ya Unaitwa Nani?* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Karuga, M.N. (2005) *Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kerlinger, F.N. (1975) *Foundations of Behavioural Research.* 3rd ed. New York Hort Rinehart and Wilston inc.

Kezilahabi, E. (1971) *Rosa Mistika.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Laurenson, D.T. na Swingewood, A. (1972) *The Sociology of Literature.* London: Macgibbon Ltd.

Maillu, D.G. (1997) *Atendaye Mema.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Manji, A. (1996) *Bonde la Wafu.* Nairobi; Phoenix.

Matundura, B. (2005) *Mwepesi wa Kusahau.* Nairobi: Phoenix.

___________(2007) *Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

___________(2013) *Hazina ya Zuena na Makombo.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

___________(2014) *Likizo ya Mkosi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbatiah, A.M. (1999) *The Origin and Development of Swahili Thesis Novel in Tanzania.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

___________(2002) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks.

Mbuthia, E.M. (2005) *A Thematic and Stylistic Analysis of Kiswahili Short Stories.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Miricho, E. et al (2008) *Distinction Kiswahili.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mkufya, W.E. (1998) *Androko na Simba.* Dar-es-Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Mpesha, N. (1996) *Children's Literature in Tanzania: A Literary appreciation of its growth and development.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (2003) *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: African Centre for Technology Studies (ACTS) Press.

Musau, P. na Pamela, N. (1997) Research in Kenyan Universities: Where are we now? Katika: Rose Marie-Beck Lutz Diegner, na Thomas Geider (wh), AAP 51. *Swahili Forum.* Afrikanistische Arbeitspapiere. Institut fiir Afrikanistik. Koln. 219-229.

Muthubi, F. (2005) *Mikakati na Mbinu za Usilimishwaji katika Fasihi ya Watoto.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ngugi, P.M. (2009) *The State of Children Literature in Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Vienna, Austria.

__________(2014) "Miaka Hamsini ya Fasihi ya Watoto Katika Kiswahili Nchini Kenya". Katika Simala, I. et al. (wh) Twaweza Communications, Nairobi 16 -33.

__________(2014) "Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia." Katika: D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (wh) *Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Studies* (TATAKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vol. 77.2014 70-180 ISBN 0856-048 X.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu,* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Rock Islands, Augustine College.

Omolo, O.L. (1967) *Tajiri Mjanja.* Nairobi: Phoenix.

Odaga, A.B. (1985) *Literature for Children and Young People in Kenya.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Orina, B.M. (2000) *Utetezi wa Maadili katika Fasihi. Nadharia ya Shaban Robert.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sommer, B. (1986) *A Practical guide to Behavioural Research Tools and Techniques.* Oxford University Press.

Swingewood, A. (1975) *The Novel and Revolution.* London: The Macmillan Press Ltd.

Thiong'o, N. (1978) "Literature in Society", in Gachukia E. na Akivaga, S.K. (mh) *Teaching of African Literature in Schools*. KLB.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Warren, A. na Wellek, R. (1973) *Theory of Literature*. London: Penguin Books.

Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

______________(2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

______________(2006) *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix.

______________(2006) *Kesi ya Kuchekesha*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

______________(2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchangunuzi wa Fasihi*. Nairobi: Video-muwa Publishers.

Wizara ya Elimu (2015) *Approved List of School Textbooks and Other Instructional Materials for Primary schools.* Nairobi.

**Kiambatisho A: Makala ya *Daily Nation***


# NATION

TSh1,700/00 : USh2,700/00 : RFr900/00) www.nation.co.ke No. 18335




# Alarm as girls top the class and boys drop out

**BY JULIUS SIGEI**
jsigei@ke.nationmedia.com

Girls are overtaking boys in nearly every level of education, a *Nation* investigation shows.

This has triggered an alarm among policy makers and education stakeholders on the effects of decades-long campaigns to promote the welfare of girls.

The findings paint a grim picture of the prospects of boys who bore the brunt of the socio-economic factors to fare badly in school. It could also have far reaching implications in homes and

**CONTINUED ON PAGE 4**

**Kiambatisho B: Jalada la *Mwepesi wa kusahau***

